# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI
## HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI.

**MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

**JUNI, 2023**

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1
2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022/2023 ........................................... 6
2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ........................................................ 7
3.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022/2023 ........................................... 8
4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO........... 47
5.0 MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024................................................................... 58
6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/2024................................................................... 66
7.0 HITIMISHO ............................................................. 66

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2022/2023 ........................................ 72

Kiambatisho Nam. 2: Maeneo yaliyorejeshewa Huduma ya Maji Safi na Salama ....................................... 74

Kiambatisho Nam. 3: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya usafishaji wa visima ......................................... 75

Kiambatisho Nam. 4: Dhana za Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Nishati iliyotayarishwa kwa ajili ya kuombewa ufadhili ..................................................................................... 76

Kiambatisho Nam. 5: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 .................................................................... 77

Kiambatisho Nam. 6: Vijiji viliyopelekewa huduma ya umeme Unguja na Pemba................................................. 78

Kiambatisho Nam. 7: Hali ya Uingizwaji na Matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa ............................................... 79

Kiambatisho Nam. 8: Mwenendo wa bei halisi na bei elekezi katika soko la Zanzibar (TZS) kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023........................................ 80

Kiambatisho Nam. 9: Idadi ya Vituo vya Mafuta vilivyopo Nchini..................................................................................... 81

Kiambatisho Nam. 10: Kiwango cha Gesi iliyoingizwa na iliyotumika Nchini (Kg)................................................... 82

Kiambatisho Nam. 11: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024...................... 83

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| GWPSA | Global Water Patnership Southern Africa |
| LPG | Liquified Petroleum Gas (Gesi ya Matumizi ya Majumbani) |
| MKUZA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| SDGs | Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu) |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TZS | Tanzania Shillings (Shilingi ya Tanzania) |
| WMNM | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZANWIP | Zanzibar Water Investment Program |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation (Shirika la Umeme la Zanzibar) |
| ZESTA | Zanzibar Energy Sector Transformation and Access (Mabadiliko ya Sekta ya Nishati Zanzibar na Upatikanaji wa umeme) |
| ZURA | Zanzibar Utility Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar) |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana hapa kwa wakati mwengine tukiwa wenye afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania kwa uongozi makini na thabiti aliouonyesha katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wake ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na juhudi zake hususan katika kuimarisha amani nchini, ukusanyaji wa kodi, utafutaji wa fedha na kuimarisha mahusiano ya kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha misingi ya usawa wa kijinsia na kuleta maendeleo katika sekta ya afya, elimu, miundombinu na maendeleo ya jamii.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza kwa vitendo ahadi zake pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025 kwa wananchi wa Zanzibar hasa katika maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo tumeshuhudia kufunguliwa kwa Miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Miradi ya Maji, Umeme, Afya, Elimu, Masoko na Uwezeshaji wa Wananchi.

4. **Mheshimiwa Spika,** kipekee niwapongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais Dk. Samia kwa kuchaguliwa na kuaminiwa na WanaCCM kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) akisaidiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar. Hii ni faraja kwetu katika usimamiaji na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

5. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema yeye na familia yake, ili kuendeleza misingi ya Utawala Bora na mshikamano katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

6. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna anavyoendelea kuchapa kazi na kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuongoza na kusimamia shughuli za Serikali katika kipindi chote cha uongozi wake. Kupitia juhudi zake, tumeshuhudia kasi ya utekelezaji wa miradi mbali mbali pamoja na mageuzi makubwa katika kuleta mafanikio kwa wananchi.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili ukiwa ni Spika wa Baraza la Kumi la Wawakilishi. Tunaimani kuwa utaendelea kusimamia vyema nafasi hiyo na utaendelea kuitumikia ipasavyo katika kuitendea haki kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

8. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, nimpongeze Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa ushupavu wake wa kukusaidia kuongoza Baraza hili. Vile vile, naomba kumpongeza Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa mchango wake mkubwa anaoutoa kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na Wizara yetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, tunawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza hili kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo. Ni imani yetu kuwa wataendelea kukusaidia katika kuendesha chombo hiki muhimu kwa maendeleo ya wananchi. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kuchaguliwa kuunda Kamati hizo. Kwa hakika, tumekua tukipokea maoni na ushauri mzuri kutoka kwao na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

10. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za pekee ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Mheshimiwa Yahya Rashid (Mamba), Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kwahani kwa busara, hekima na uzoefu wake anaoutumia katika kuiongoza Kamati hii. Kwa

hakika busara, hekima na uzoefu wake alionao ndio ngao iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kuweza kutatua changamoto mbali mbali katika jamii zinazohusu sekta ya Maji, Nishati na Madini. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Khuzaima Mbarak Tahir Mwakilishi wa Viti Maalum Vijana Mkoa wa Mjini kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

11. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Shaaban Ali Othman Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae na Naibu Waziri katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Hakika amekuwa akinisaidia sana na kunishauri katika kusimamia Wizara hii na kuongeza kasi ya usimamizi bora wa huduma za maji, nishati na madini kwa wananchi.

12. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi kuiongoza Wizara hii inayomgusa kila mwananchi katika maisha yake ya kila siku. Naahidi nitaitumikia nafasi hii kwa nguvu zangu zote katika kuwaletea maendeleo wananchi na kuhakikisha huduma za maji, umeme, mafuta na maliasili zisizorejesheka zinapatikana na zinaimarika kwa kiwango kikubwa.

13. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Manaibu Waziri walioteuliwa na wanaoendelea na nafasi zao katika Wizara mbali mbali. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

14. **Mheshimiwa Spika,** pia, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazolikabili Jimbo letu.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nikishukuru Chama Changu cha Mapinduzi (CCM) kwa namna kinavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 katika kuhakikisha Zanzibar inapiga hatua kubwa za maendeleo. Wizara inaahidi kuendelea kutekeleza programu zake kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021/2026 na miongozo inayoendelea kutolewa na Serikali.

16. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu niwasilishe Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Programu na Shughuli za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022/2023

***Bajeti na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini yake zimetekeleza Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ilivyoidhinishwa katika Baraza lako Tukufu Mwezi Juni, 2022 na imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) chini ya Fungu N03. Programu Kuu ni:-

i. ***Programu Kuu:*** Usimamizi wa Huduma za Maji,
ii. **Programu Kuu:** Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini, na
iii. ***Programu Kuu:*** Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM.

18. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hizi, umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020-2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004, Sera ya Nishati ya Mwaka 2009, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 (Africa Agenda 2063), Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDG 2030), Ahadi alizozitoa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha Kampeni za Uchaguzi, Vipaumbele vya

Mheshimiwa Rais, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na Maagizo ya Utendaji kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu aliyoyatoa wakati wa kuwaapisha na maelekezo na miongozo mbalimbali inayoendelea kutolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

## 2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

19. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 135,334,521,000** kwa kazi za matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 1,512,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 5,117,400,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 128,705,021,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

20. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 Wizara imeingiziwa jumla ya **TZS. 38,992,854,380** sawa na asilimia 29 ya fedha zote kwa kazi za kawaida na Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla ya **TZS. 684,588,300** Sawa na asilimia 45 kwa matumizi mengineyo, **TZS. 6,206,154,721** sawa na asilimia 121 kwa ajili ya mishahara na **TZS. 32,102,111,359** sawa na asilimia 25 kwa miradi ya maendeleo. **Kiambatisho Namba. 1 kinafafanua**.

### *Ukusanyaji wa mapato ya Serikali*

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS. 10,514,947,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na malipo ya maliasili zisizorejesheka ambapo

kwa kipindi cha miezi tisa makadirio ya makusanyo yalikua ni **TZS. 8,037,710,500**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023, Wizara imekusanya Jumla ya **TZS. 9,816,306,401** sawa na asilimia 122 ya makusanyo hayo.

## 3.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022/2023

22. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini yalikuwa ni pamoja na; kufanya tafiti za maji zinazohusu mabadiliko na athari za tabianchi, kufanya utafiti wa njia mbadala ya kuzalisha maji safi na salama (uvunaji wa maji ya mvua na maji yaliyo chini ya bahari), kuandaa kanuni na miongozo ya namna ya kudhibiti maji safi na maji machafu pamoja na miongozo ya uunganishaji wa umeme kwenye gridi ya Taifa, kuandaa na kufanya mapitio ya Sera na Sheria mbali mbali za Wizara na kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar.

### *MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI*

23. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai-Machi, 2022/2023, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi kama ifuatavyo: -

***Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji***

24. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS. 106,703,257,000** kwa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 252,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 156,716,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 3,608,300,000** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara na **TZS. 102,686,241,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

25. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 programu hii iliingiziwa Jumla ya **TZS. 35,745,075,068** sawa na asilimia 33 ya fedha zote. Kati ya hizo **TZS. 152,798,401** sawa na asilimia 61 kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 136,292,620** sawa na asilimia 87 kwa ajili ya mishahara, **TZS. 4,397,115,376** sawa na asilimia 122 kwa ajili ya ruzuku ya mshahara na **TZS. 31,058,868,671** sawa na asilimia 30 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Hali ya Maji Nchini**

26. **Mheshimiwa Spika,** maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya viumbe vyote vinavyoishi duniani. Maendeleo yote duniani ikiwa ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa yanategemea upatikanaji wa huduma ya maji. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa mstari wa mbele kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma ya maji safi na salama.

27. **Mheshimiwa Spika,** sekta ya maji inakumbwa na ongezeko la mahitaji ya maji kunakochochewa na ongezeko la idadi ya watu, kukua kwa miji pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo uwekezaji na utalii, mabadiliko ya tabianchi, uvamizi wa vianzio vya maji, uchakavu wa miundombinu ya maji na mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia huduma ya maji, vyote hivyo vinaipa changamoto kubwa sekta ya maji.

28. **Mheshimiwa Spika,** matumaini yetu kwamba Wazanzibari wote tunaweza kushirikiana katika kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya maji nchini iwapo kwa pamoja tutaamua kubadili mitazamo yetu tuliyonayo na kukubali kuwa mchango wa kila mmoja ni wa muhimu katika kufanikisha azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi Mijini na Vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, Serikali inaendelea kujenga, kukarabati, kusambaza mitandao ya maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji Nchini.

30. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2023 hali ya uzalishaji maji nchini imeendelea kuimarika ambapo wastani wa uzalishaji wa maji umefikia asilimia 67 kwa Unguja na Pemba ikilinganishwa na asilimia 56 iliyofikiwa mwezi Machi, 2022. Aidha, mahitaji ya maji nchini yameendelea kukua ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 mahitaji ya maji yamefikia lita 240,465,120 kwa siku na uzalishaji ni lita

146,926,338 kwa siku hivyo kupelekea kuwa na upungufu wa lita 93,538,782 kwa siku.

31. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kukamilika kwa utekelezaji wa miradi mbali mbali ya Sekta ya Maji nchini, kiwango cha uzalishaji maji kinatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 75 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2023.

32. **Mheshimiwa Spika,** kiwango hicho cha maji kitatokana na kukamilika kwa miradi mipya inayohusisha uchimbaji wa visima vipya na ufungaji wa pampu katika visima vikongwe, ujenzi na ukarabati wa matangi ya kuhifadhia maji pamoja na upanuzi wa mtandao wa maji. Hatua hizo zitapelekea kuimarika kwa huduma ya maji kwa wananchi wa Zanzibar.

33. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, hali ya miundombinu na mitandao ya usambazaji maji inaendelea kuimarika kulingana na viwango vya ubora wa maji vya Kitaifa licha ya kuwepo kwa changamoto ya uchakavu wa mtandao wa maji katika baadhi ya maeneo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea na hatua za ulazaji wa mtandao mpya wa mabomba ya maji na kubadilisha mabomba chakavu.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali pamoja na washirika wa maendeleo kuhusiana na kuwekeza katika uimarishaji wa miundombinu ya maji kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wananchi na wawekezaji.

35. **Mheshimiwa Spika,** napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama

kuendelea kutoa ushirikiano katika kuchangia, ni vizuri wananchi wakatambua kwamba michango yao ni muhimu katika kuifanya huduma ya maji kuwa ya uhakika na endelevu.

## A. IDARA YA MAENDELEO YA MAJI

36. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Maendeleo ya Maji inajukumu la kusimamia maendeleo ya sekta ya maji na kuhakikisha kwamba huduma za maji safi na salama zinapatikana kwa uhakika na endelevu. Vile vile, Idara ina jukumu la kufuatilia ubora wa rasilimali maji, usalama wa vyanzo vya maji pamoja na kufanya tafiti za maendeleo ya rasilimali maji.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inaimarisha ufuatiliaji na upatikanaji wa taarifa za kila siku za mwenendo wa rasilimali maji katika visima, Idara ya Maendeleo ya Maji inatarajia kuanzisha mfumo wa Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Taarifa za visima (Data loger) katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Mfumo huo utabainisha uchakataji wa taarifa zilizokusanywa (Data Analysis) na kutafsiri taarifa hizo kwa kuangalia viwango vya maji (Water Level) na mkandamizo wa maji (Water Pressure) katika visima.

38. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2023 Wizara imefanikiwa kufanya ukaguzi katika vyanzo 26 vya maji Unguja na Pemba ili kupata taarifa zitakazosaidia kubainisha namna bora ya uendeshaji wa mfumo huo. Kukamilika kwa mfumo huo, kutasaidia kupata taarifa za mwenendo wa uzalishaji wa maji (Water Production) na kupelekea kuwepo kwa huduma endelevu ya maji.

39. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Idara mbali mbali za Wizara, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Taasisi ya "Global Water Partnership"-Tanzania (GWP-TZ) inaendelea na kazi ya utayarishaji wa Mkakati wa Mahitaji ya Maji Zanzibar. Kwa sasa hatua inayoendelea ni ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wadau wa sekta ya maji.

40. **Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mkakati huo, kutasaidia kupanga na kuweka miongozo sahihi katika sekta ya maji kwa kuzingatia matumizi na mahitaji ya rasilimali maji kwa mujibu wa shughuli za watumiaji wa rasilimali maji.

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji imefanikiwa kuandaa Warsha ya Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji (Zanzibar Water Investment Programme – ZanWIP 2022/2027). Lengo la Warsha hiyo ni kutoa uelewa wa namna ya kuhuisha mipango na mikakati ya Taasisi za Serikali katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali maji nchini. Aidha, kupitia warsha hiyo wadau wa taasisi hizo walisisitiza umuhimu wa kushirikishwa kikamilifu katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango huo, ili kuifanya rasilimali hiyo kuwa endelevu.

42. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji iliadhimisha Kitaifa kilele cha Siku ya Maji Duniani mnamo tarehe 22 Machi, 2023. Maadhimisho hayo yalifanyika kwa kutekeleza zoezi la upandaji wa miti katika eneo la

Bumbwisudi pamoja na vyanzo vyengine vya maji. Jumla ya miti 1,770 ya asili na matunda ilipandwa katika vyanzo vya maji kwa Unguja na jumla ya miti 850 ilipandwa kwa upande wa Pemba. Matarajio yetu kuwa zoezi hili la upandaji wa miti litasaidia katika uhifadhi na ulindaji wa vyanzo vya maji pamoja na kuepusha uvamizi unaotokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Wizara inasimamia utekelezaji wa Miradi ya maji ipasavyo, Idara ya Maendeleo ya Maji imefanikiwa kufanya tathmini ya kina ya miradi ya maji iliyowahi kutekelezwa Zanzibar kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita (1990 hadi 2020). Lengo la tathmini hiyo ni kubaini changamoto za kitaalamu zilizojitokeza na hatimae kutoa ushauri Serikalini juu ya namna bora ya utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kwa sasa na itakayokuja baadae.

44. **Mheshimiwa Spika,** miradi iliyofanyiwa tathmini ni:-

i. Zanzibar Rural Water Supply (1997-1999). Mfadhili wa ***Mradi; Abudhabi Fund,***
ii. Zanzibar Urban and Rural Water Supply and Sanitation (2009-2013). ***Mfadhili wa Mradi; AfDB,***
iii. Zanzibar Urban Water and Sanitation Project (2013-2019). ***Mfadhili wa Mradi; AfDB,***
iv. Zanzibar Drilling and Water Supply Project (2013-2018). ***Mfadhili wa Mradi; People's Republic of China*** na
v. China Aid Zanzibar Water Supply Project (2018-2020). ***Mfadhili wa Mradi; People's Republic of China***.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa na vyanzo mbadala vya maji safi na salama, Wizara imekamilisha hatua za utayarishaji wa Hadidu Rejea kwa ajili ya kumtafuta mshauri elekezi atakayefanya upembuzi yakinifu kuhusiana na uibuaji wa vyanzo mbadala vya maji katika maeneo makuu mawili (2) ambayo ni; uvunaji wa maji ya mvua (Rain water harvest) na ubadilishaji wa maji ya bahari kuyafanya maji matamu (Desalination).

46. **Mheshimiwa Spika,** upembuzi huo utasaidia kupata taarifa za gharama za uwekezaji pamoja na kuibua maeneo ya utekelezaji wa mradi. Shughuli hiyo inatarajiwa kutekelezwa kwa ushirikiano baina ya Tume ya Mipango Zanzibar na Wizara Maji, Nishati na Madini.

### *B. MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)*

47. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) pamoja na mambo mengine inajukumu la kuzalisha na kusambaza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ZAWA ilipanga kukusanya jumla ya **TZS. 7,312,115,801** kutokana na mapato yake ya ndani. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023, jumla ya **TZS. 2,333,226,229.61** sawa na asilimia 32 ya makadirio zimepatikana kutokana na mapato ya ndani.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakisha huduma ya maji safi na salama inapatikana kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba, Wizara kupitia ZAWA imefanikiwa kununua pampu mpya na kuziweka katika visima vilivyokuwa na hitilafu. Jumla ya pampu 103 zimefungwa katika visima 33 vya Unguja na 70

kwa Pemba na kupelekea uzalishaji wa maji safi na salama kuongezeka katika maeneo mbali mbali nchini. **Kiambatisho Namba 2** kinahusika.

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA inaendelea na jitihada za kuwafikishia wateja huduma ya maji safi na salama, ili kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma ya maji nchini. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, ZAWA imefanikiwa kuwasajili na kuwaunganisha jumla ya wateja wapya 3,664 sawa na asilimia 61 ya wateja 6000 waliopangwa kusajiliwa na kuunganishwa na mtandao huo kwa Unguja na Pemba. Kati ya wateja hao 2,254 kwa Unguja na wateja 1,410 kwa Pemba.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa ZAWA inawatambua wateja wake pamoja na kurahisisha ukusanyaji wa mapato, imeanza kazi ya kuziunganisha mita zote kwenye mfumo wa (Geographical Information System - GIS MAP). Jumla ya mita 5,557 za wateja zimeunganishwa katika mfumo wa GIS MAP pamoja na zoezi la kuhakiki taarifa za wateja wa Mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo awamu inayofuata ni kwa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja.

51. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, ZAWA imefanikiwa kufunga mita za pre-paid kwa kushirikiana na Kampuni ya Padma Smart Technology Limited ya Bangladesh. Jumla ya mita janja (Smart Meter) 11 zimefungwa, kati ya hizo 10 zimefungwa bandarini na moja (1) Ofisi Kuu ya Mamlaka ya Maji Mabuluu ikiwa ni sehemu ya majaribio. Zoezi hilo limepangwa kuendelea katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Ufungaji wa mita hizo umepelekea udhibiti wa matumizi ya maji yasiyo ya lazima na kuimarisha ukusanyaji wa mapato unaoendana na hali halisi ya kiwango cha matumizi ya maji hayo.

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imeendelea na zoezi la kufanya upanuzi wa mtandao wa maji kwa kulaza mabomba mapya na kuondoa mabomba chakavu, ili kuongeza upatikanaji wa maji katika maeneo mengi zaidi na kupunguza idadi kubwa ya maji yanayopotea pamoja na mivujo itokanayo na kupasuka kwa mabomba. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, ZAWA imefanikiwa kulaza mabomba yenye urefu wa mita 30,239 katika maeneo ya Unguja na Pemba ambapo mita 20,459 kwa Unguja na mita 9,780 kwa Pemba.

53. **Mheshimiwa Spika,** maeneo ambayo yamenufaika na ulazaji wa mabomba mapya ni Wilaya ya Kaskazini "B" mita1,650, Wilaya ya Magharibi "A" mita 5,116, Wilaya ya Magharibi "B" mita 2,256, Wilaya ya Kati mita1,900, Wilaya ya Mjini mita 9,537 na Wilaya ya Micheweni mita 9,780.

54. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, ZAWA imefanikiwa kupunguza upotevu wa maji (non-revenue water) katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Jumla ya mivujo 812 iliripotiwa, kati ya hiyo, mivujo 395 kwa Unguja na 417 kwa Pemba imezibwa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika kushajihisha jamii juu ya usimamizi endelevu wa rasilimali maji nchini, Wizara kupitia ZAWA imefanikiwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi bora ya maji, uchangiaji wa huduma ya maji na usajili wa

wateja katika maeneo ya Wilaya ya Mjini Unguja na Wilaya ya Mkoani, Wete na Micheweni kwa Pemba.

56. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, ZAWA imefanya mikutano katika ngazi ya Shehia juu ya mfumo mpya wa ulipaji wa huduma ya maji kwa njia ya mtandao na usimamizi wa rasilimali maji (Zan-Malipo) kwa maeneo ya Machomane-Fletini, Matale, Chuchuu, Ukutini, Kiuyu-Minungwini na Kiuyu-Kigorofani.

57. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya utoaji wa elimu hiyo, yameongeza mwamko kwa wananchi hasa katika maeneo ya mjini juu ya kulipia huduma ya maji safi na salama. Jitihada hizo zimefanyika kwa lengo la kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa kulipia huduma ya maji na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

58. **Mheshimiwa Spika,** aidha, ZAWA imefanikiwa kutayarisha na kurusha hewani vipindi 14 kupitia Redio Jamii Mkoani, Assalaam, Plus Radio na Hits FM, vipindi saba (7) kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC - TV) pamoja na matukio 9 ya kihabari. Vipindi hivyo vilikuwa na maudhui juu ya maendeleo ya Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar pamoja na Mradi wa maji kupitia fedha za ahueni ya Uviko-19 ambavyo vimetanabahisha umma juu ya hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali yao katika kuimarisha suala la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama pamoja na kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa kulipia huduma hiyo.

59. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA inaendelea kupokea na kutatua malalamiko ya wananchi kuhusiana na utoaji wa huduma zake kupitia mifumo inayohusisha mitandao ya kijamii ya ZAWA ikiwemo tovuti ya "Instagram", "Facebook", "WhatsApp", "Twitter" na "Youtube" pamoja na mtandao wa Sema Na Rais (SNR). Jumla ya malalamiko 98 kuhusiana na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama yameripotiwa kwenye mfumo wa SNR kati ya hayo 49 yamepatiwa ufumbuzi na 49 yanaendelea kufanyiwa kazi.

60. **Mheshimiwa Spika,** pia Wizara kupitia ZAWA imefanikiwa kufanya ukarabati na usafishaji wa chemchem pamoja na visima vinavyotoa huduma kwa wananchi. Kwa upande wa chemchem ukarabati huo umefanyika katika Chemchem ya Mwanyanya na Mtopepo. Kadhalika, jumla ya visima 60 vimesafishwa ambapo visima 33 kwa Unguja na 27 kwa Pemba. Kiambatisho Namba 3 kinahusika.

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) ambao utaonyesha uhalisia wa kupata vyanzo vya maji katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba. Tayari Mshauri Elekezi ameshaanza kazi kwa upande wa Pemba na Ripoti ya Awali (Inception Report) imeshawasilishwa kwa Kamati ya Uongozi ya Wizara.

## MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

### *Programu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini*

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS. 26,757,321,000** kwa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 285,800,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 452,741,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 26,018,780,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 programu hii iliingiziwa jumla ya **TZS. 1,677,403,673** sawa na asilimia 6 ya fedha zote. Kati ya hizo **TZS. 50,611,414** sawa na asilimia 18 kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 583,549,570** sawa na asilimia 129 kwa ajili ya mishahara na **TZS. 1,043,242,689** sawa na asilimia 4 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:-

### A. IDARA YA NISHATI NA MADINI

65. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini ina jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusiana na Nishati na Madini. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 Idara ilipanga kutekeleza majukumu yake kwa

kuzingatia Mpango kazi wa mwaka wa fedha 2022/2023 na kupata mafanikio yafuatayo:-

66. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa na chanzo chake cha kuzalisha umeme, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) tayari imeshafunga mkataba wa mauziano ya umeme (PPA) na Kampuni ya Generation Capital Ltd. Kampuni hiyo ina lengo la kuwekeza katika nishati ya umeme wa jua kwa kujenga mtambo wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 180 kwa kipindi cha miaka isiyopungua 25 ambapo kwa awamu ya kwanza itazalisha megawati 30 kwa Unguja katika eneo la Bambi ndani ya kipindi kisichopungua miezi sita tokea kusainiwa kwa mkataba huo. Vile vile, Wizara imetiliana saini Mkataba wa Uzalishaji wa umeme na Kampuni ya ESR ya Ujerumani ambayo itazalisha Megawati 15 za umeme wa jua kwa ajili ya kisiwa cha Pemba.

67. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mikataba hiyo ya uzalishaji umeme baina ya ZECO na Kampuni hizo kutaiwezesha Zanzibar kuwa na vyanzo vya kujitegemea vya uzalishaji wa umeme kama ilivyoelekeza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025.

68. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na ZECO ipo katika hatua za kumpata Mshauri Elekezi atakaefanya kazi ya Upembuzi Yakinifu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme na kutafuta ufumbuzi wa changamoto ya umeme mdogo katika baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba.

69. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba wananchi wanaepukana na matumizi mabaya ya nishati pamoja na kutunza mazingira, Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imeendelea kutoa elimu juu ya matumizi bora ya nishati mbadala ya umeme kwa jamii kupitia Maonyesho ya Nane Nane yaliyofanyika Kizimbani na Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi zilizofanyika Maisara.Elimu hiyo imelenga kuwaongezea wananchi uelewa wa matumizi bora ya nishati pamoja na utunzaji wa mazingira kwa kuacha kukata miti kwa ajili ya kupata Nishati ya kupikia.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imetayarisha dhana za miradi (Concept Notes) zitakazoweza kuisaidia Serikali kutatua changamoto za nishati Zanzibar. Idara imefanikiwa kuandaa jumla ya dhana za miradi saba (7) zinazoonekana katika **Kiambatisho namba 4**.

### *B. SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)*

71. **Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa huduma ya umeme Zanzibar inaendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya uniti **430,252,267.72 kWh** zimeuzwa kati ya **404,760,728.00 kWh** zilizopangwa sawa na asilimia 106 ya mauzo na kupelekea makusanyo ya jumla ya **TZS. 117,583,679,018.17** ambayo pia yamejumuisha na tozo ya VAT.

72. **Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya umeme (Power consumption) yameendelea kukua na kuongezeka kwa wastani wa Megawati kumi na tano (15MW) baina ya mwaka 2021 hadi 2023. Mahitaji ya juu ya umeme (Peak demand) kwa upande

wa Unguja yamefikia Megawati 104.9 (matumizi katika waya wa megawati 100 yamefikia megawati 83, na waya wa megawati 45 yalifikia megawati 21.9) sawa na asilimia 72 ya uwezo wa waya mbili zilizopo yaliyofikiwa tarehe 31 Januari 2023. Aidha, kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme ni Megawati 12 (12MW) sawa na asilimia 60 ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa Megawati 20.

73. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na Zanzibar kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara ipo haja ya kuwa na njia mbadala ya upatikanaji wa nishati hiyo, ili kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa huduma hiyo. Hali hii inatokana na ukuaji wa sekta za kiuchumi na kijamii kunakosababishwa na ukuwaji wa sekta ya utalii, viwanda na biashara, na kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa umeme nchini.

74. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, mpango wa kutafuta vyanzo mbadala vya kuzalisha umeme unakwenda sambamba na mpango mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020-2050 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 chini ya kifungu namba 175 kwa kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika inayojitegemea kupitia upanuzi wa vyanzo mbali mbali vya nishati mbadala.

75. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Zanzibar haiathiriki na kiwango cha juu cha mahitaji ya Umeme (Peak demand), Wizara kupita ZECO imefanikiwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya waya wa zamani wa chini ya bahari (Submarine Cable) yenye uwezo wa Megawati 45 (45MW). Kutokana na ukarabati huo, waya huo tayari umeshaanza

kupokea wastani wa megawati 23 (23MW) za umeme. Aidha, ZECO inaendelea kufanya ukarabati wa transfoma za miundombinu hiyo, ili kuweza kufikia kiwango cha Megawati 35 (35MW) kitakachotumika kwa waya wa zamani.

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha kilovolti 33 na kilovolti 11. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya urefu wa mtandao wa kusafirisha umeme umefikia kilomita 1,645 sawa na ongezeko la asilimia 18.9 ikilinganishwa na kilomita 1,383 zilizokuwa zimefikiwa mwezi Machi, 2022. Kati ya hizo, njia za msongo wa kilovolti 33 ni kilomita 213.61 na kilovolti 11 ni kilomita 48.39.

77. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kujenga njia za umeme mdogo wa msongo wa 400V wenye urefu wa kilomita 83.28 sawa na asilimia 58 kati ya makadirio ya njia iliyopangwa kujengwa ya kilomita 144. Ongezeko hili limetokana na mahitaji ya ujenzi wa njia kuu na idadi kubwa ya wateja wanaoungiwa umeme.

78. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wote wa Zanzibar, Wizara kupitia ZECO inaendelea na kazi ya kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023 ZECO imekusanya **TZS. 124,970,290,909.14** sawa na asilimia 96 ya makadirio yaliyowekwa ya **TZS. 130,409,873,260**.

79. **Mheshimiwa Spika,** makusanyo hayo yametokana na mauzo ya umeme pamoja na mapato mengineyo ikiwemo gharama za uungaji wa wateja wapya na malimbikizo ya madeni. Kutokufikiwa kwa lengo hilo, kumetokana na kutokulipwa kwa wakati matumizi ya huduma ya umeme.

80. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha miundombinu ya Umeme, ili wananchi waweze kupata huduma ya uhakika na endelevu. Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023 ZECO ilipanga kutumia **TZS. 7,920,000,000** kwa kazi za uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme. Katika utekelezaji wa kazi hizo, ZECO imetumia **TZS. 6,142,467,622.21** sawa na asilimia 78 ya fedha zote.

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 ZECO ilipanga kubadilisha jumla ya nguzo mbovu 2,040 kwa Unguja na Pemba, hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya nguzo mbovu 2,137 zimebadilishwa ambazo ni sawa na asilimia 104 ya malengo yaliyowekwa. Vile vile, ZECO imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Transfoma 1,036 kati ya 1,374 kwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 75 ya transfoma zilizopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Aidha, kupitia ukaguzi huo, ZECO imefanikiwa kurekebisha jumla ya transfoma 40 zilizobainika kuwa na hitilafu (35 kwa Unguja na tano (5) kwa Pemba).

82. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia ZECO inaendelea kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata umeme wa uhakika na katika kiwango kinachoridhisha. Katika kufanikisha hilo, ZECO imeimarisha upatikanaji wa kiwango

cha umeme katika maeneo 49 sawa na asilimia 66 ya maeneo 74 yaliyopangwa kurekebishwa. Kwa upande wa Unguja maeneo 37 na maeneo 12 kwa Pemba yamerekebishwa. ***Kiambatisho Namba. 5 kinatoa ufafanuzi zaidi***.

83. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mikakati ya kuhakikisha wananchi wote wanaungiwa umeme na wanafaidika na huduma za umeme nchini. Kupitia azma hiyo ZECO imefanikiwa kuongeza idadi ya wateja wapya kwa kuwaunganishia huduma hiyo. Jumla ya wateja 25,216 sawa na asilimia 74 ya wateja 34,500 waliokadiriwa kuunganishiwa umeme kwa Unguja na Pemba ambapo Unguja wateja 20,884 na Pemba wateja 4,332 wamepatiwa huduma hiyo.

84. **Mheshimiwa Spika,** idadi ya wateja wapya wanaounganishiwa umeme imeongezeka zaidi kutokana na Serikali kupunguza gharama za kuunganisha umeme pamoja na kufidia gharama za uvutaji wa laini na uwekaji nguzo kutoka kwa wananchi kuweza kubebwa na Serikali.

85. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kusambaza huduma ya umeme katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Jumla ya vijiji 59 vimenufaika na huduma hiyo, kati ya hivyo vijiji 39 kwa Unguja na vijiji 20 kwa Pemba. **Kiambatisho Namba. 6** kinatoa ufafanuzi zaidi.

86. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kupunguza upotevu wa umeme kwa asilimia 0.6 kutoka asilimia 15.6 iliokuwepo mwaka 2021/2022 hadi kufikia asilimia 15.0 kwa mwaka 2022/2023. Kupungua kwa upotevu huo kumesababishwa na jitihada mbali mbali

zilizofanywa na ZECO ikiwemo kufanya ukaguzi wa wateja mara kwa mara, kubadilisha mita mbovu na zilizopitwa na wakati pamoja na kufunga mita zinazojisoma wenyewe (AMR).

## C. MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

87. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inajukumu la kudhibiti huduma za maji na nishati, ili huduma hizo zipatikane kwa kiwango bora na chenye uhakika. Kufuatia jukumu hilo Wizara imepiga hatua kubwa katika kudhibiti nishati pamoja na mafuta na gesi kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii.

88. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 15,947,436,329** ambazo ni sawa na asilimia 122 ya makadirio ya **TZS. 13,024,721,654** yaliyopangwa kukusanywa katika kipindi hicho. Makusanyo hayo yanatokana na tozo za mafuta na mapato mengineyo (leseni, adhabu na malipo ya uuzaji wa zabuni).

89. **Mheshimiwa Spika,** sababu zilizopelekea kuongezeka kwa makusanyo hayo ni pamoja na kuongezeka kwa uingizaji wa mafuta na kuongezeka kwa matumizi ya mafuta yaliyosababishwa na ongezeko la harakati za kiuchumi.

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 ZURA ilipanga kutumia jumla ya **TZS. 15,179,704,166.** Makadirio ya matumizi hayo

yanajumuisha matumizi ya kawaida **TZS. 9,853,904,166**, matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo **TZS. 825,800,000** pamoja na **TZS. 4,500,000,000** ambazo ni mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023, ZURA ilitumia jumla ya **TZS. 11,050,698,726** sawa na asilimia 73 ya makadirio ya matumizi kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo **TZS. 5,018,905,279.76** zilitumika kwa kazi ya kawaida, **TZS. 231,793,445.86** kwa kazi za miradi ya maendeleo, **TZS. 1,300,000,000** matumizi katika mfuko wa fidia na **TZS. 4,500,000,000** ambazo ni mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**91. Mheshimiwa Spika,** sababu zilizopelekea kupungua kwa matumizi katika kipindi hicho ni pamoja na kufutwa kwa shughuli za Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (CRC) katika kutekeleza Agizo la Serikali Kuu.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kudhibiti huduma za maji na nishati Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kuandaa Kanuni na miongozo ya namna ya kudhibiti huduma za maji na nishati. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 ZURA imefanikiwa kukamilisha Tafsiri ya Kanuni ya Utoaji Vibali kwa mafundi wanaojishughulisha na uwekaji wa mifumo ya Umeme (Electrical Installation Permit Regulations) pamoja na kupitia na kutafsiri kanuni ya usimamizi wa vituo vya mafuta 2022 (Petroleum Filling Station Regulations). Aidha, Kanuni nyengine zilizopitiwa ni Kanuni ya Utoaji wa Leseni za Usambazaji Maji na kupitia Kanuni ya uingizaji wa mafuta kwa pamoja (BPS).

93. **Mheshimiwa Spika**, kadhalika, Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kuandaa Rasimu ya Kanuni ya Tozo na kuiwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa marekebisho ya mwisho kwa ajili ya kusainiwa na Mheshimiwa Waziri. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 ZURA imefanya mapitio ya Sheria ya ZURA Na. 7 ya mwaka 2013 kutokana na uhitaji wa Sheria hiyo. Hatua inayofuata ni kuwasilishwa Sheria hiyo katika ngazi ya Wizara na kuiwasilisha Tume ya kurekebisha Sheria.

94. **Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu na kuimarisha mifumo ya Mamlaka, ZURA imetoa mafunzo ya mfumo wa udhibiti (ZIRS) kwa wadau wa ndani na wa nje, ili kutoa uelewa kwa wadau hawa. Aidha, mfumo huo umewezesha ZURA kukusanya na kupokea maoni na mapendekezo ya wadau pamoja na kufanyiwa kazi.

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kukamilisha utafiti unaohusiana na Gharama ya Uendeshaji wa Huduma za Maji kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (Cost of Service Study of ZAWA). Vile vile, ZURA imekamilisha uandaaji wa dhana (Concept Notes) kwa ajili ya utafiti wa kutathmini uwezo wa kumudu bei na miundo ya gharama ya gesi ya kupikia katika soko la Zanzibar na utafiti wa uelewa wa jamii kuhusu huduma zinazotolewa na ZURA. Tafiti hizo inalenga kuimarisha huduma za sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka.

96. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai- Machi, 2022/2023 Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kudhibiti kikamilifu huduma za maji na nishati (mafuta, umeme, na gesi ya kupikia- LPG).

Katika udhibiti wa huduma za maji, ZURA imekagua vyanzo vya maji 43 kwa upande wa Unguja, kati ya hivyo vyanzo 19 vipo katika Wilaya za Mkoa wa Kaskazini. Kupitia ukaguzi huo imebainika kuwa vyanzo vilivyopo katika maeneo yote yaliyokaguliwa yalikidhi viwango vya ubora wa matumizi ya binadamu.

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa vyanzo vya maji 131 pamoja na miundombinu iliyokaguliwa Pemba imebainika kwamba asilimia 50.4 ya vyanzo vilivyokaguliwa vilikosa uzio. Vile vile, mita za kupimia uzalishaji wa maji katika vyanzo 56 kati ya 131 zilizokaguliwa zilikuwa zimeharibika.

98. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imekamilisha uandaaji wa viashiria vitakavyotumika katika kupima utendaji kazi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Viashiria hivyo vitatumika kuandaa mkataba wa utendaji kazi (Perfomance Contract) baina ya ZURA na ZAWA.

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa udhibiti wa huduma ya umeme, Wizara kupitia ZURA imefanikiwa kukagua jumla ya vituo vya umeme 41 pamoja na njia za kusambazia umeme katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Lengo la ukaguzi huo ni kutambua hali halisi ya huduma inayotolewa kwa wananchi. Vile vile, ZURA ilikagua miundombinu ya kusambazia umeme katika Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo jumla ya transfoma 35 kati ya 40 zilizopangwa kukaguliwa. Aidha, katika maeneo yaliyoonekana na mapungufu Wizara kwa kushirikiana na ZURA imepeleka taarifa ya maaeneo hayo kwa Taasisi husika na tayari hatua za maboresho zinaendelea.

100. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 Wizara kupitia ZURA imefanya zoezi la ukusanyaji wa taarifa za matumizi ya majenereta ya kuzalisha umeme wa dharura lililofanyika katika Mahoteli na baadhi ya Taasisi, ambapo jumla ya majenereta 80 yameorodheshwa kwa upande wa Unguja. Zoezi hilo lilikua na lengo la kutambua na kupata taarifa za mifumo zitakazosaidia Mamlaka katika uendeshaji wa shughuli zake.

101. **Mheshimiwa Spika,** faida za ukusanyaji wa taarifa hizo ni kuiwezesha Wizara kuwa na kanzidata (database) ya wazalishaji umeme wa dharura kwa kutumia jenereta, kujua kiwango cha umeme wa dharura kilichopo nchini na kuwaweka katika utaratibu watumiaji wa majenereta kwa mujibu wa Kanuni (0-10kW), (11kW-250kW) na (250kW na kuendelea) pamoja na kuwapatia leseni wazalishaji waliozidi Kilowati 250.

102. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kuratibu shughuli za uingizwaji wa mafuta kwa pamoja (BPS), kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, ZURA imewapatia mafunzo watendaji wa kitengo cha BPS juu ya uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji. ZURA imekamilisha Muongozo wa Taratibu za Ushushaji wa Mafuta (Standard Operating Procedure-SOP).

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai - Machi 2022/2023, ZURA ilipanga kuingiza mafuta lita 135,652,174, hadi kufikia Machi, 2023, mafuta yaliyoingizwa yalifikia lita 165,955,023. Mafuta hayo huingizwa na kampuni ya GBP kupitia mfumo wa Uingizwaji wa Mafuta kwa pamoja (BPS) na kusambazwa

kwa kampuni nne (4) ambazo ni; GAPCO, PUMA, UGL na ZPL. **Kiambatisho Namba.7** kinafafanua.

104. **Mheshimiwa Spika,** ZURA kwa mujibu wa Sheria Nam. 7/2013 inajukumu la kupanga na kutangaza bei elekezi za mafuta kwa Zanzibar. Bei hizo hutolewa kila mwezi kwa mujibu wa mabadiliko ya bei katika Soko la Dunia. **Kiambatisho Namba. 8** kinahusika.

105. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha mafuta na gesi yanayoingizwa nchini yanatosheleza, Wizara kupitia ZURA iliendelea na jukumu la uchukuaji wa takwimu za upokeaji wa Mafuta pamoja na ufuatiliaji wa mauzo kwenye Bohari (Depot) na vituoni, ili kuelewa kiwango cha akiba kilichopo kwenye Bohari pamoja na matumizi halisi ya kila siku kwa kila bidhaa ya Mafuta.

106. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ina jumla ya Bohari sita (6) za kuhifadhia mafuta, tano (5) kwa Unguja na moja (1) Pemba. Aidha jumla ya vituo vya mafuta vinavyouza mafuta reja reja ni 96, kati ya hivyo 77 Unguja na 19 Pemba. **Kiambatanisho Namba. 9** kinafafanua.

107. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kampuni ya United Petroleum (UP) imejenga Bohari mpya iliyopo Mangapwani yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya lita 21,000,000 za Mafuta ikiwemo Petroli lita 8,000,000, Diseli lita 8,000,000, Mafuta ya Ndege lita 4,000,000 na Mafuta ya Taa lita 1,000,000. Bohari hiyo ina uwezo wa kuhifadhi mafuta ya matumizi ya wastani wa mwezi mmoja kwa upande wa Unguja. Awali kampuni hiyo ya United Petroleum (UP) ilikuwa inatumia matangi ya Serikali

yaliyopo katika Bohari (Depot) ya Mtoni ambayo uwezo wake wa kuhifadhia mafuta ni mdogo sana.

108. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA hufanya ukaguzi wa uwekaji alama katika mafuta (Petroleum Marking System), kwa kipindi cha Julai - Machi 2022/2023, jumla ya mafuta yaliyowekewa alama ni lita 131,108,022. Ukaguzi huo umegundua vituo viwili (2), kituo cha Dunga Service Station (ZP) na kituo cha New Kwerekwe Petro Station kukosekana kwa alama baada ya kufanyiwa ukaguzi, ZURA imetoa adhabu ya kulipa faini ya **TZS. 3,000,000** kwa kila kituo. Aidha, kwa upande wa Pemba hakukuwa na kituo kilichoingiza mafuta kinyume na utaratibu au uchanganyaji wa bidhaa moja ya mafuta na nyengine na hakuna kituo kilichokosa alama baada ya kufanyiwa ukaguzi.

109. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imeendelea kudhibiti sekta ndogo ya gesi kwa waingizaji na wasambazaji wa bidhaa hiyo inayotumika majumbani. Kampuni zinazoingiza na kuuza gesi kwa jumla katika visiwa vya Zanzibar ni tano (5), zikiwemo Oryx Gas Tanzania Limited, TP Company Limited (V-Gas), Lake Gas Limited, Taifa Gas Tanzania Limited na Al Nabahan Gas Supply (O-Gas).

110. **Mheshimiwa Spika,** kiwango cha gesi inayotumika majumbani kilichoingia nchini kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 ni kilogramu 5,981,877 na kiwango cha matumizi kimefikia kilogramu 6,070,784 kwa Unguja. Aidha, kwa upande wa Pemba gesi iliyoingizwa imefikia kilogramu 244,035 na kutumika kilogramu 250,859. **Kiambatanisho Namba. 10** kinafafanua.

111. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imeendelea kutoa elimu kwa umma iliyowashirikisha wafanyabiashara wa jumla na rejareja wa gesi ya kupikia pamoja na matumizi salama ya gesi hiyo. Aidha, mafunzo hayo yalitoa miongozo juu ya kuweka mahitaji muhimu ya kiusalama ikiwemo vifaa vya kuzimia moto (fire extinguisher), mizani, alama za tahadhari na bango la bei katika maduka yao.

112. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu masuala ya udhibiti wa huduma za maji na nishati, Wizara kupitia ZURA imetoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na makongamano ya kijamii, pamoja na kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati kwa kurusha hewani vipindi vitatu (3) vya TV na sita (6) vya Redio. Vipindi hivyo vililenga kutoa uelewa juu ya usalama katika vituo vya mafuta, matumizi sahihi na salama ya gesi ya kupikia (LPG) na utaratibu wa malalamiko kwa huduma zinazodhibitiwa.

## *C. MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MADINI*

113. **Mheshimiwa Spika,** Wizara, kupitia Idara ya Nishati na Madini imeendelea kusimamia sekta ya madini kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla **TZS. 9,816,306,401** sawa na asilimia 122 ya **TZS. 8,037,710,500** ambazo zimepangwa kukusanywa kwa miezi tisa. Ongezeko la mapato hayo yametokana na kuongezeka kwa uhitaji mkubwa wa maliasili zisizorejesheka unaotokana na utekelezaji wa miradi mingi ya Serikali, kukuwa kwa Sekta ya Utalii na udhibiti wa upotevu wa mapato yanayotokana na maliasili hizo.

114. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inaimarisha utoaji wa huduma, kupitia Idara ya Nishati na Madini imeanzisha madawati maalum katika ngazi za Wilaya kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kufanya maombi ya vibali kupitia mfumo (Madini Management System).

115. **Mheshimiwa Spika,** mfumo huo umesaidia kuondoa mrundikano wa maombi ambayo yalikuwa yakichukua muda mrefu mpaka muombaji kupatiwa kibali. Kwa sasa mwananchi anapata kibali cha maliasili zisizorejesheka ndani ya masaa nane ya kazi mara tu baada ya kukamilisha taratibu za maombi.

116. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini inaendelea kutafuta rasilimali mbadala wa Maliasili zisizorejesheka, kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya CCM ya 2020/2025. Hadi sasa Wizara imekamilisha Upembuzi Yakinifu (feasibility study) wa uingizaji wa madini ya ujenzi kutoka nje ya Zanzibar kwa lengo la kupunguza uchimbaji ambao umeonekana kuathiri shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kimazingira. Upembuzi huo, utaiwezesha Zanzibar kutumia madini ya ujenzi kutoka nje na kuvilinda visiwa vyetu na athari zinazotokana na uchimbaji wa Maliasili zisizorejesheka.

117. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara imepokea na kulifanyia kazi ombi la Kampuni ya Zan Sand Co. Ltd ambayo inazalisha mchanga unaotokana na kusaga mawe. Mradi huo unasaidia kupunguza athari kubwa katika maeneo ya uchimbaji mchanga unaosababisha uharibifu wa mazingira.

118. **Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti uchimbaji holela wa Maliasili zisizorejesheka, Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imeendelea kudhibiti uchimbaji holela wa Maliasili katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ambapo hufanya doria za kila siku pamoja na doria za kushitukiza hususan nyakati za usiku katika maeneo ya Wilaya za Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Kati ambayo yanayoripotiwa zaidi vitendo hivyo vya uchimbaji.

119. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na shughuli za uchimbaji wa Maliasili Zisizorejesheka. Shughuli za uchimbaji wa Maliasili hizo unaenda sanjari na uharibifu wa mali za wananchi ikiwemo mazao na vipando vyengine. Wizara imeweza kulipa jumla ya **TZS. 469,552,992** kwa waathirika mbalimbali katika mwaka wa fedha 2022/2023.

120. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inatekeleza vyema Ibara ya 151 (b) ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020/2025 inayoitaka Wizara kufanya matumizi mbadala ya maeneo ya mashimo yaliyochimbwa mchanga na kifusi, ili kuleta tija kiuchumi na kijamii, pamoja na kuweka vizuri haiba ya maeneo hayo. Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imeanza utekelezaji wa Mpango wa Uhuishaji wa maeneo matano yenye ukubwa wa hekari 104 yaliyochimbwa mchanga na Serikali.

121. **Mheshimiwa Spika,** hadi sasa jumla ya maeneo mawili yamehuishwa (Shehia ya Pangatupu) ambapo jumla ya miche 40,000 imepandwa katika maeneo hayo. Aidha, Wizara imeweza kuwasimamia vizuri wachimbaji binafsi katika

kuhuisha maeneo yao ambapo jumla ya maeneo manne yameweza kuhuishwa.

122. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Taasisi ya Geological Survey of Tanzania (GST) inaendelea na kazi ya utayarishaji wa Ramani ya Kijiolojia ambayo itasaidia kubaini aina ya miamba na rasilimali zinazopatikana katika miamba yote iliyopo Zanzibar. Kwa sasa Wizara inaendelea na utafiti wa awali katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba na kukamilisha mpango kazi wa utengenezaji wa ramani hiyo.

123. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imedhamiria kuimarisha ukaguzi wa madini Bandarini na Viwanja vya Ndege, ili kudhibiti uingizaji na utoaji madini nchini. Katika kutekeleza hilo, Wizara tayari imeshaandika barua kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar pamoja na Mamlaka ya Bandari kwa lengo la kupatiwa Ofisi ya Ukaguzi wa Madini yanayoingizwa na kutolewa Zanzibar. Wizara inaendelea kufuatilia Taasisi husika pamoja na ununuzi wa vifaa, ili vituo hivyo vianze kutoa huduma rasmi.

***Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM***

124. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Ofisi Kuu Pemba.

125. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS. 1,873,943,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara. Kati ya hizo **TZS. 974,300,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 899,643,000** kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023 programu hii iliingiziwa Jumla ya **TZS. 1,570,375,640** sawa na asilimia 84 ya fedha zote. Kati ya hizo **TZS. 481,178,485** sawa na asilimia 49 kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 1,089,197,155** sawa na asilimia 121 kwa ajili ya mishahara.

126. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu hii kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:-

### *A. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI*

127. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inaendelea kutekeleza shughuli zake ipasavyo, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeandaa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano (2023/2028). Mpango huo umezingatia muongozo mpya kutoka Tume ya Mipango na Vipaumbele vya Wizara ikiwemo uimarishaji wa huduma ya maji safi na salama, upatikanaji wa huduma za nishati za uhakika pamoja na maliasili zisizorejesheka kwa maendeleo ya Zanzibar.

128. **Mheshimiwa Spika,** mpango huo tayari umeshajadiliwa katika kikao cha Kamati Tendaji ya Wizara pamoja na vikao vya wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao, hatua inayofuata ni kuuwasilisha Tume ya Mipango na hatimae kuukamilisha

ndani ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kukamilika kwa mpango huo kutaiwezesha Wizara kuwa na malengo mkakati na kujipima kwa ufanisi katika kutekeleza vipaumbele vyake kwa kipindi husika.

129. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa takwimu katika kufanya maamuzi sahihi ya majukumu, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya vikao kazi viwili (2) kwa maafisa takwimu wa Wizara kwa lengo la kuwapatia uelewa wa namna ya kukusanya taarifa na kuzichambua kulingana na Taasisi na Idara zao. Vikao hivyo vilifanywa kwa kushirikiana na Maafisa Takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

130. **Mheshimiwa Spika,** Maudhui ya vikao hivyo ni kuandaa tathmini ya mahitaji ya takwimu (Statistical Needs Assessment) kupitia Sekta zilizo chini ya Wizara ambayo itapelekea kuandaliwa kwa kitabu cha takwimu (Statistical Abstract) kwa kila mwaka.

131. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inaandaa na kutoa miongozo madhubuti juu ya namna bora ya matumizi ya nishati, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Nishati ya Zanzibar kwa kuzingatia muongozo mpya uliyotolewa na OMPR juu ya uandaaji wa Sera zote za Zanzibar. Sera hiyo imeshawasilishwa katika kikao cha Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi za Wizara kwa ajili ya kuipitia na kuimarisha, ili iendane na mahitaji na matumizi ya huduma za nishati kwa sasa na baadae. Kukamilika kwa Sera hiyo kutaongeza uwezo kwa Wizara na Serikali juu ya kuwa na miongozo madhubuti itakayoimarisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za Nishati Zanzibar.

132. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) chini ya Mradi wa "Institutional Support Domestic Resource Mobilization and Natural Resource Governance" (ISPDRMNRG), Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inaendelea na maandalizi ya Sera ya Madini ya Zanzibar. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kukamilisha taratibu za manunuzi na zabuni kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kuandaa sera hiyo. Ripoti ya uchambuzi imewasilishwa Benki ya Afrika kwa ajili ya kumteua mzabuni alieshinda na kuweza kukabidhiwa kazi hiyo.

133. **Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa Sera hiyo, kutapelekea kuandaliwa kwa Sheria na Kanuni za Madini Zanzibar. Hatua hiyo itaiwezesha na kuipa uwezo Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini kusimamia kikamilifu shughuli za upatikanaji, usafirishaji, uzalishaji na uuzaji wa madini ya vito ikiwemo almasi, dhahabu pamoja na madini ya ujenzi (mawe, mchanga, kifusi na kokoto).

134. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji safi na salama inaendelea kuimarika Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi kupitia ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto Duniani (UNICEF) inaendelea na kazi ya kuifanyia mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004, ili iendane na kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii juu ya mahitaji na matumizi ya huduma hiyo. Maoni ya wadau kuhusiana na Sera hiyo yamekusanywa, hatua inayoendelea ni kuchakata na kuchambua maoni hayo, ili kukamilisha uandaaji wa ripoti ya awali ya Sera Mpya ya Maji ya Zanzibar ya mwaka, 2023.

135. **Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa Sera hiyo, kutapelekea kuendana na mabadiliko na hali halisi iliyopo sasa katika Sekta ya Maji. Pia, Sera hiyo itatoa miongozo baina ya Wizara na ZAWA juu ya utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana, inaimarika na inawafikia wananchi kwa wakati. Kadhalika, kutaimarisha na kutoa fursa kubwa kwa wawekezaji ambao watakuwa na nia ya kuwekeza katika Sekta ya Maji.

136. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati iliyomo katika ZanWIP, ili wananchi wa Zanzibar waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. Mnamo tarehe 14 – 15, Septemba, 2022 Wizara iliandaa Kongamano la Kimataifa la Maji Zanzibar (Zanzibar Water conference) lililojadili Maandiko mbali mbali ya tafiti zinazohusiana na Sekta ya Maji, Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (ZanWIP), Changamoto zinazoikabili sekta ya maji kwa Zanzibar pamoja na kutoa fursa kwa washirika wa maendeleo ambao wataonyesha nia ya kuwekeza katika Sekta ya Maji Zanzibar.

137. **Mheshimiwa Spika,** kongamano hilo lilizinduliwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kupitia kongamano hilo, washirika wa maendeleo wamejitokeza na kuonesha nia ya kusaidia kuimarisha Sekta ya Maji wakiwemo GIZ ya Ujerumani.

138. **Mheshimiwa Spika,** kwa kufanikisha hilo, Wizara iliandaa mapendekezo ya Miradi katika Sekta ya Maji na kuyawasilisha kwa washirika wa maendeleo (GIZ) na kujadiliwa katika kikao

kilichofanyika Ujerumani, ili kuweza kutoa mchango wao katika kuimarisha sekta hii nchini. Matokeo ya uwasilishaji huo, GIZ wamekubali kusaidia utekelezaji wa miradi itakayofanyika ndani ya mwaka huu wa fedha 2023/2024.

139. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara inaendelea na jitahada za kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya maji na kuhakikisha kuwa mafanikio katika utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (ZanWIP) yanapatikana, ili kufikia malengo yaliyopangwa. Katika kufikia hilo, tarehe 08 Februari, 2023 WMNM iliandaa Mkutano wa Washirika wa Maendeleo (Donors Round table Meeting) ambao ulihudhuriwa na wadau kutoka nchi na Taasisi tofauti wakiwemo Washirika wa maendeleo, wawekezaji na wawakislishi kutoka Taasisi za Serikali.

140. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la mkutano huo ni Wizara kujadiliana na washirika hao juu ya utekelezaji wa ZanWIP, kuwasilisha maeneo ya vipaumbele vya uwekezaji katika sekta ya maji, ili waweze kutoa mchango wao (kiufundi na kifedha) katika kufikia malengo yaliyopangwa. Kufuatia kikao hicho, baadhi ya Washirika wa Maendeleo wakiwemo KfW, GIZ, TBI, JICA pamoja na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) walioonesha nia ya kusaidia uimarishaji wa sekta ya maji Zanzibar.

141. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara hii imefanya ufuatiliaji kwa kufanya ziara ya kukagua maeneo mbali mbali yanayotekelezwa miradi kwa Unguja na Pemba. Lengo la ziara hizo ni kukagua hatua za utekelezaji zilizofikiwa katika miradi hiyo kulingana na makubaliano ya mikataba husika.

Vile vile, kukagua kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo, ili kuona inaendana na muda uliowekwa na itakamilika kwa wakati.

142. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi inayofadhiliwa kupitia fedha za ahueni ya Uviko – 19, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa miradi hiyo inaendelea na iko katika hatua nzuri za utekelezaji licha ya kuwepo kwa changamoto zinazopelekea kuzorotesha kasi ya utekelezaji wake. Hata hivyo, Wizara iliwataka wakandarasi pamoja na washauri elekezi wa miradi hiyo kuhakikisha wanatatua changamoto zilizo ndani ya uwezo wao na zile zilizo nje ya uwezo wao zitafanyiwa kazi na Wizara, ili kukamilisha miradi hiyo kwa wakati. Maeneo yaliyokaguliwa juu ya ujenzi wa matangi ni; Mgeni Haji, Bumbwini, Tumbatu, Unguja Ukuu na Bambi kwa Unguja na kwa Pemba ni Chanjaani, Kendwa, Shumbamjini/ Kilindini, Makangale/Konde na Pujini.

143. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, ziara kama hiyo imefanyika katika maeneo yanayochimbwa visima kupitia fedha za ahueni ya Uviko – 19. Maeneo hayo ni; Mgenihaji, Bambi, Kiashange, Donge Kipange, Unguja Ukuu, Kipandoni na Kaburikikombe kwa Unguja pamoja na maeneo ya Chanjaani, Kironjo, Mtuhaliwa, Makangale, Tumbe, Mbiji, Manyaga, Kipapo na Konde kwa upande wa Pemba. Katika ziara hiyo imebainika kuwa visima vyote 38 (11 Unguja na 27 Pemba) vimeshachimbwa visima 11 Unguja na visima 27 Pemba vishafanyiwa majaribio.

144. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maagizo ya Viongozi wetu Wakuu (SMZ na SMT) juu ya kuwepo na ushirikiano katika Sekta zisizokuwa za Muungano, Wizara imeendelea

kuimarisha ushirikiano uliopo katika Sekta ya Maji kati yake na Wizara ya Maji ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni kutokana na kufanyika kwa vikao vya ushirikiano mara kwa mara kwa lengo la kubadilishana uzoefu juu ya uimarishaji wa Sekta ya Maji.

145. **Mheshimiwa Spika,** vikao hivyo, hufanyika kwa kuzingatia pande zote mbili za Muungano (Zanzibar na Tanzania Bara) kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 jumla ya vikao viwili (2) vimefanyika vyenye lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza masuala mbali mbali yanayohusiana na Sekta ya Maji. Vikao hivyo vilifanyika kati ya tarehe 30/8 hadi 02/9/2022 Mkoa wa Tanga na Pwani na kati ya tarehe 21 hadi 25/11/2022 Bonde la Rufiji-Iringa.

146. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano huu unaendelea kuleta tija kwa pande zote mbili za Muungano, kwa sasa kumekuwa na utamaduni wa kubadilishana uzoefu kwa kuazimana wataalamu kuja kusaidia utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo na kufanya tafiti za masuala ya maji kadiri inavyohitajika.

147. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ushirikiano katika Sekta ya Nishati na Madini, Wizara ipo katika hatua za kutiliana saini Hati za Makubaliano na Wizara husika za SMT kwa lengo la kuimarisha Ushirikiano katika Sekta hizo.

### *B. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI*

148. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia maendeleo ya Rasilimali Watu na utekelezaji wa kazi za kila siku za Ofisi ikiwemo; kuimarisha mazingira ya kazi, kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, miongoni mwa stahiki hizo ni pamoja na mishahara, likizo, malipo baada ya saa za kazi, kutoa ubani kwa wafiwa, malipo ya kujikimu na malazi pamoja na stahiki nyenginezo.

149. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, jumla ya wafanyakazi 136 wamelipwa mishahara yao pamoja na kulipiwa michango yao ya ZSSF, wafanyakazi 29 wamekwenda likizo ya kawaida, wafanyakazi 32 wamelipiwa ada ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Aidha, wafanyakazi 100 wamenufaika na mafunzo mbali mbali ya Kiidara ikiwemo Mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Mafunzo ya Athari za Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na mafunzo ya Uandaaji wa Usimamizi wa Miradi. Vile vile, Wafanyakazi watano (5) wamepandishwa daraja kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

150. **Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza ufanisi kazini Wizara imefanikiwa kuwafanyia tathmini ya utendaji kazi wafanyakazi wake, ili kujua kwa kiasi gani wanatekeleza majukumu yao ipasavyo, jumla ya wafanyakazi 88 wamefanyiwa tathmini kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023. Tathmini hiyo ya mara kwa mara inapelekea kuongeza kasi ya utendaji kazi kwa wafanyakazi. Pia, Idara imefanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu na kuuwasilisha Wizara husika kwa hatua zinazofuata.

151. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, Wizara imefanikiwa kuendesha jumla ya vikao (11) vya Bodi ya Zabuni, vikao sita (6) vya Kamati Tendaji na Vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi. Aidha, Wizara imeandaa vikao viwili (2) vya Kamati ya Ukaguzi na Ukaguzi wa Hesabu wa Awali na Endelevu katika Ofisi na Idara zote za Wizara pamoja na vikao (3) vya wafanyakazi. Sambamba na hilo, Wizara imefanya manunuzi ya vitendea kazi, ili kuboresha mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

**C. AFISI KUU – PEMBA**

152. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba, Wizara inaendelea na hatua za kuimarisha Mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi, pamoja na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Miongoni mwa stahiki hizo ni Mishahara, mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, likizo, malipo ya kujikimu na malazi na stahiki nyenginezo pamoja na kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa Wizara kwa upande wa Pemba.

153. **Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu – Pemba ina jumla ya wafanyakazi 44. Kati ya hao, Wanaume 28 na Wanawake 16. Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023, Afisi Kuu - Pemba imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli zote zinazotekelezwa na Taasisi zilizopo chini ya Wizara (ZAWA, ZECO na ZURA). Vile vile, Afisi kuu Pemba imefanikiwa kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kukagua maeneo mbali mbali ya uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka, ujenzi wa matangi, visima, ulazaji wa mabomba pamoja na maeneo yaliyopelekewa umeme.

154. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa maliasili zisizorejesheka zinaratibiwa vyema, Afisi Kuu - Pemba imeendelea kufanya doria za usiku na mchana, ili kuzuia upotevu wa mapato na kuzuia uharibifu wa mazingira pamoja na kuratibu uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka katika kware zote zilizopo kisiwani Pemba. Doria hizi husaidia wananchi kutunza mazingira pamoja na kuimarisha upatikanaji wa mapato ya Serikali kwa wakati sahihi.

155. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Afisi Kuu - Pemba imefanya kikao kilichowajumuisha wakusanyaji wa mapato (Check Point), kitengo cha ZAN-MALIPO, kitengo cha mapato kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango pamoja na Wakaguzi wa Hesabu kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Matokeo ya Kikao hicho yalipelekea mafanikio makubwa kwa Wizara juu ya ukusanyaji wa mapato.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

*156.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023 Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo na kupata mafanikio yafuatayo;

***i. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar***

157. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar unagharimu USD 92.18 Milioni sawa na **TZS. bilioni 211.83** ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Exim ya India. Katika kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023

mradi huu umetumia **TZS 26,796,444,654** sawa na asilimia 67.02 ya makadirio ya **TZS. 39,977,960,600** ya mwaka kutoka katika fedha za washirika wa maendeleo. Aidha, kwa upande wa Serikali Jumla ya **TZS. 2,500,000,000** sawa na 71.42 zimetumika kati ya makadirio ya ***TZS 3,500,000,000*** ya fedha zilizotengwa kwa upande wa Serikali.

158. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023 Mamlaka ya Maji kupitia Mradi huu imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo;

**1) Uchimbaji wa visima**

159. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2023, ZAWA kupitia mradi huu imefanikiwa kwa asilimia 100 kukamilisha kazi ya uchimbaji wa visima 64 katika maeneo ya Dole (8), Kidutani (14), Dimani (5), Mfenesini (10) Maungani (9), Mkorogo (8) na Masingini (10).

**2) Ujenzi wa matangi**

160. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Ujenzi wa matangi yote 15 ya kuhifadhia maji umefikia wastani wa asilimia 87 ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) umefikia wastani wa asilimia 76. kwa upande wa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) umefikia wastani wa asilimia 91, na LOT 3 (Kidutani na Masingini) ujenzi wa matangi umefikia wastani wa asilimia 94, kazi za ukamilishaji wa matangi hayo zinaendelea.

**3) Ulazaji wa mabomba**

161. **Mheshimiwa Spika,** kazi ya ulazaji wa mabomba kwa mradi mzima imefikia wastani wa kilomita 418.33 kati ya kilomita

466.9 sawa na asilimia 90 ya makadirio ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) zimefikia kilomita 164, LOT 2 (Mkorogo, Maungani na Dimani) kilomita 140 na LOT 3 (Kidutani na Masingini) kilomita 113.

**4) Kazi ya uhakiki na ulipaji wa fidia**

162. **Mheshimiwa Spika,** kazi ya uhakiki na ulipaji wa fidia kwa waathirika wa mradi imefanyika kwa maeneo ya Kizimbani, Bumbwisudi, Mfenesini, Jumbi na Vuga Mkadini. Aidha, kazi ya ujenzi wa jengo la ofisi umefikia wastani wa asilimia 85.

***ii. Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji Zanzibar kupitia fedha za ahueni ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO - 19 kwa Upande wa ZAWA***

163. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar Serikali ilitenga jumla ya **TZS. Bilioni 34,200,000,000** kupitia fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya kutekeleza programu ya kuhuisha ustawi wa uchumi na kijamii kutokana na athari za UVIKO-19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

164. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2023, Mamlaka ya Maji kupitia mradi huu imetumia Jumla ya **TZS 13,255,987,910.7** sawa na asilimia 38.8 ya fedha zote kwa kazi za utekelezaji wa mradi ikiwemo malipo kwa watoa huduma na wakandarasi.

165. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulilenga kuendeleza kazi za uchimbaji wa visima (38), ukarabati wa visima (36), ununuzi wa pampu 123, uboreshaji na ubadilishaji wa mabomba chakavu kwa masafa ya kilomita 319, ujenzi wa Matangi

mapya (10) na ukarabati wa Matangi makongwe (2) na ujenzi wa vibanda 52 vya kuhifadhia pampu kwa Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 kazi zilizofanyika ni kama zifuatazo;

### 1) Uchimbaji wa Visima

**166. Mheshimiwa Spika,** jumla ya visima 11 Unguja vimeshakamilika na tayari vimeshafanyiwa majaribio katika maeneo ya Mgeni haji (2), Kaburi Kikombe (1), Kipandoni (1) Unguja Ukuu (2), Bambi (2), Donge Kipange (2) na Kiashange (1).

**167. Mheshimiwa Spika, Aidha,** visima 27 kwa upande wa Pemba vimechimbwa katika maeneo ya Kiuyu Manda (2), Saninga (1), Kilindini (3), Kijuki (1), Uwondwe (1), Kiungoni (1), Mbiji (2), Manyaga (1), Mtuhaliwa (1), Ng'ambwa (3), Mjimbini (1), Junguni (1), Kengeja (1), Chambani (1), Mkanyageni (1), Jaani (1), Chanjaani (1), Kiwani (1), Ng'ombeni (1) na Ngwachani (1) na Shamiani (1). Kazi ya uchimbaji wa visima na kuvifanyia majaribio (Pumping test) imekamilika kwa asilimia 100.

### 2) Ujenzi wa Matangi

**168. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla ujenzi wa matangi 10 umefikia wastani wa asilimia 86.4 kwa Unguja na Pemba, ambapo ujenzi wa matangi matano (5) kwa Unguja umefikia wastani wa asilimia 91.8 na matangi matano (5) kwa Pemba umefikia wastani wa asilimia 81. Aidha, kazi ya ukarabati wa matangi mawili (2) ya Saateni na Mnara wa mbao imefikia asilimia 100 kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo.

### Ujenzi wa Matangi matano (5) Unguja

| Nam | Mkoa | Wilaya | Eneo | Hatua ya Ujenzi (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kusini | Kati | Bambi-Uroa | 97 |
| 2 | | Kati | Mgenihaji | 97 |
| 3 | | Kati | Unguja Ukuu | 92 |
| 4 | Kaskazini | Kaskazini B | Bumbwini | 95 |
| 5 | | Kaskazini A | Tumbatu | 78 |
| **Wastani** | | | | **91.8** |

### Ujenzi wa Matangi matano (5) Pemba

| Nam | Mkoa | Wilaya | Eneo | Hatua ya Ujenzi (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kusini | Chake Chake | Chanjaani | 95 |
| 2 | | Chake Chake | Pujini | 90 |
| 3 | | Mkoani | Kiwani | 90 |
| 4 | Kaskazini | Michweni | Shumbamjini | 70 |
| 5 | | Michweni | Makangale | 60 |
| **Wastani** | | | | **81** |

### 3) Uchimbaji wa Misingi na ulazaji wa mabomba

169. **Mheshimiwa Spika,** Kazi ya uchimbaji wa misingi ya mabomba inaendelea kwa Unguja ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya mita 17,483 zimekamilika kati ya 174,017 sawa na asilimia 10 kwa Unguja na Pemba, Kazi ya uchimbaji wa misingi ya ulazaji wa mabomba inaendelea ambapo hadi Machi jumla ya mita 87,316 zimekamilika kati ya 145,173 sawa na asilimia 60. Kazi ya upimaji wa maeneo ya kulazwa mabomba Unguja na Pemba imekamilika kwa asilimia 100. Aidha, kazi ya ujenzi wa vibanda 52 vya kuhifadhi mitambo ya kuendeshea pampu inaendelea katika hatua za mwisho kwa Unguja na Pemba.

### 4) Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya maji

170. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya Pampu 123 za kusukumia maji, zimeshapokelewa na kuanza kutumika, aidha pampu nyengine 72 zimeshafika bandarini Zanzibar, majenereta 11 tayari yameshafika na yanaendelea kutumika, Mashine 13 za kuungia bomba tayari zimeshafika na kuanza kutumika, Vifaa vya upimaji seti 4 na Gari 2 za uchimbaji wa visima (RIGS) tayari vimeshafika Bandarini Zanzibar na hatua za utoaji zinaendelea.

### 5) Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Huduma ya Maji na Miundombinu ya Maji (Intergrated Water Management System)

171. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Huduma ya Maji na Miundombinu ya Maji. Mfumo huo umetayarishwa kwa ushirikiano na Chuo cha Maji cha Dar es Salaam utakaoiwezesha ZAWA kupata taarifa juu ya maeneo yaliopo wateja wake (Customer mapping), maeneo yaliopita miundombinu ya maji (Infrastructure mapping), kubaini mivujo na taarifa za upotevu wa maji (Water Leakage Information), ujazo wa Matangi ya maji, (Water tank level), na kudhibiti ubora wa rasilimali maji (Water quality monitoring).

172. Mheshimiwa Spika, Hadi sasa, ZAWA imekamilisha zoezi la kuwatambua wateja 106,842 kwa Mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo wateja 30,455 - Wilaya ya Mjini, 36,089 – Magharibi A na 40,298 Magharibi B tayari wamefanyiwa uhakiki na

kuingizwa kwenye Mfumo pamoja na usajili wa wateja wapya.

iii. ***Mradi wa Upembuzi Yakinifu juu ya Usalama wa Maji na Kina cha Maji chini ya Ardhi (Kfw)***

173. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi kampuni ya CES-Consulting Engineers kutoka nchini Ujerumani inaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa kujua hali ya usalama na upatikanaji wa maji kwa Visiwa vya Unguja na Pemba.

174. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unagharimu jumla ya EURO 660,000 sawa na wastani wa **TZS. 1,700,000,000** zinatumika kwa ajili ya utafiti. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu imeshawasilishwa na ripoti ya awamu ya pili inatarajiwa kuwasilishwa mwishoni mwa mwezi Juni 2023. Aidha, mradi huu unategemewa kukamilika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024.

iv. ***Mradi wa Utambuzi wa visima binafsi pamoja na uangalizi wa ubora wa maji unaotekelezwa kwa pamoja baina ya ZAWA na Shirika la UNICEF***

175. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na UNICEF inaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa visima binafsi Unguja na Pemba, zoezi hilo lilianza rasmi mwezi Disemba 2022 na linategemewa kukamilika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mradi huu unafadhiliwa na UNICEF kwa gharama ya **TZS. 247,000,000**.

**176. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Machi, 2023, jumla ya visima 16,425 vimetambuliwa katika zoezi hili, kwa upande wa Pemba jumla ya visima 3,795 vimetambuliwa na zoezi limekamilika na kwa upande wa Unguja jumla ya visima 12,630 na zoezi linaendelea. Jadweli ifuatayo inafafanua mchanganuo wa visima vilivyotambuliwa kwa ngazi ya Wilaya.

| Namb. | Wilaya | Visima Vilivyotambuliwa |
|---|---|---|
| 1 | ChakeChake | 1,138 |
| 2 | Kaskazini A | 283 |
| 3 | Kaskazini B | 528 |
| 4 | Kati | 1,401 |
| 5 | Kusini | 125 |
| 6 | Magharibi A | 2,715 |
| 7 | Magharibi B | 6,798 |
| 8 | Micheweni | 847 |
| 9 | Mjini | 780 |
| 10 | Mkoani | 1,060 |
| 11 | Wete | 750 |
| **Jumla ya Visima** | | **16,425** |

***v. Mradi wa Uimarishaji wa Huduma Endelevu za maji safi na salama Zanzibar (USD 35 -Exim Bank India).***

**177. Mheshimiwa Spika,** Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya EXIM ya India na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, jumla ya USD Milioni 35 zimepangwa kutumika kutoka Benki ya EXIM. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi huu ulipangiwa jumla ya **TZS. 1,090,700,000** ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa mradi na **TZS. 11,385,000,000** kutoka kwa Muhisani kwa ajili ya malipo ya awali kwa Wakandarasi wa mradi na ulipaji wa fidia na

gharama za uendeshaji wa mradi.

178. **Mheshimiwa Spika,** Hadi sasa, hatua iliyofikiwa katika mradi huu ni kufanya mapitio ya Ripoti ya Usanifu wa Mradi (DPR) ambapo zoezi hili linategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2023 na baadae kuwasilishwa Benki ya EXIM ya India kwa ajili ya kupata kibali (No Objection) cha kuendelea na hatua nyengine za ujenzi.

***vi. Mradi wa Uendelezaji visima vilivyochimbwa kupitia mradi wa Ras- Al- Khaimah***

179. **Mheshimiwa Spika,** Kazi ya uendelezaji wa miundombinu ya visima vya Ras-al-khaimah zipo katika hatua za mwisho ambapo jumla ya visima 32 vimeweza kuendelezwa kupitia Programu ya Uviko-19 kati ya visima 56 vilivyokua vimebakia hapo awali na hivyo kufanya bakaa ya visima 23 ambavyo havijaendelezwa.

***vii. Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundo mbinu ya Umeme Zanzibar (Capacity Building on Maintenance Project) - (CBMP)***

180. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO chini ya Mradi wa (CBMP) imefanikiwa kuzifanyia matengenezo laini kubwa za umeme zenye mkondo wa kilovolti 33 pamoja na kubadilisha nguzo mbovu kwa Unguja na Pemba.

181. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi, 2022/2023 ZECO imefanikiwa kujenga njia za umeme mkubwa zenye urefu wa kilomita 9 ambapo kilomita 5 zimejengwa

kutoka Mwanyanya hadi Mtoni Mazrui na kilomita 4 kutoka Msikiti Ngamia hadi kituo cha Welezo. Kadhalika, jumla ya mita mbovu 1,372 zimebadilishwa kwa Unguja na mita 623 kwa Pemba.

***viii. Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati (Zanzibar Energy Sector Transformation and Access - ZESTA)***

182. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya umeme Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na ZECO inaendelea na hatua za utekelezaji wa ZESTA. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 mradi wa ZESTA umetekelezwa na kupata mafanikio yafuatayo;

183. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imekamilisha taratibu za manunuzi za kumpata mshauri elekezi wa kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kusafirishia umeme yenye uwezo wa 132kV kwa kilomita 100 kuanzia Welezo kupitia Ubago na kuelekea Kaskazini (Matemwe) na Kusini (Makunduchi) Unguja. Njia hiyo itasaidia kutatua changamoto za umeme ikiwemo tatizo la umeme mdogo na upotevu wa umeme kwa maeneo ya Kaskazini na Kusini Unguja.

184. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tatizo la mahitaji makubwa ya umeme linapungua, Wizara kupitia ZECO imekamilisha taratibu za kumpata mshauri elekezi atakaesimamia kazi za kumtafuta na kumsimamia mjenzi wa mtandao wa udhibiti wa mfumo wa umeme (SCADA). Mfumo huo utarahisisha mawasiliano ya vituo vya umeme, miundombinu ya usafirishaji na ugawaji umeme na kubaini kwa wepesi hitilafu za kiufundi zitakapojitokeza katika mfumo

wa umeme kwa lengo la kufanya marekebisho.

185. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imekamilisha taarifa ya uthamini wa mali za wananchi kwa maeneo yatakayopitiwa na mradi kwa lengo la kulipa fidia stahiki. Aidha, Wizara imekamilisha utaratibu wa kumpata mshauri elekezi ambae ataratibu zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika kutokana na utekelezaji wa mradi ili kutimiza masharti ya Benki ya Dunia katika ulipaji wa fidia.

***ix. Mradi wa Kuijengea Uwezo Sekta ya Nishati (Zanzibar Energy Sector Support - ZESS)***

186. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulijumuisha kazi zifuatazo:- Utoaji wa mafunzo kwa watendaji wa Wizara na ZECO, Ununuzi wa kifaa cha upimaji wa Mita (Meter Test Bench), Kuunganisha mifumo ya Bili na Ununuzi wa mita za TUKUZA pamoja na Mita zinazojisoma wenyewe (AMR). Aidha, kazi zote tayari zimeshatekelezwa kwa kiasi kikubwa ambapo shughuli iliyobakia ni ukamilishaji wa ufungaji wa mita 16 za AMR kwa wateja wakubwa.

187. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023 Jumla ya mita 98 za (AMR) zimefungwa ambapo kati ya hizo mita 74 zimefungwa katika maeneo ya Unguja na mita 24 kwa Pemba. Aidha, Mradi huu unatarajiwa kukamilika rasmi ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ufungaji wa mita 16 za AMR zilizosalia.

x. ***Mradi wa Usambazaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme Zanzibar kupitia fedha za ahueni ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO-19 kwa Upande wa ZECO***

188. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza mradi huu Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar imepatiwa jumla ya TZS. 11.469 milioni za ununuzi wa vifaa vya umeme kwa lengo la kuwafikishia huduma ya umeme wananchi wa Unguja na Pemba.

189. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kuwaungia umeme wateja wapya 493 (Unguja) na 80 (Pemba) wenye uhitaji wa nguzo ambao wamekamilisha taratibu za uunganishaji huduma ya umeme. Kadhalika, kwa upande wa wateja wasio na mahitaji ya nguzo Shirika limeshawaungia huduma ya umeme jumla ya wateja 14,340 (Unguja) na 1,857 (Pemba). Aidha, Shirika limesambaza huduma ya umeme katika vijiji 43 kwa upande wa Unguja na vijiji 21 kwa upande wa Pemba.

## 5.0 MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

190. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

   i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya Maji, Nishati na Madini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati pamoja na kufanya mapitio ya Sera, Sheria na miongozo ya utoaji wa huduma hizo;

ii. Kuendeleza tafiti za maji pamoja na njia mbadala za kuzalisha maji safi na salama;
iii. Kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa ajili ya mitambo ya kusambazia maji safi na salama ili kukidhi mahitaji ya wananchi;
iv. Kusimamia masuala ya nishati Zanzibar pamoja na Kushiriki katika masuala ya nishati Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
v. Kuendelea na utafutaji wa Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar;
vi. Kuongeza ufanisi kwa kuwapatia huduma bora wananchi;
vii. Kuongeza wateja wapya kwa kusambaza huduma ya maji na umeme katika maeneo mapya na
viii. Kuondoa changamoto katika maeneo ambayo yana uhaba wa maji na umeme mdogo.

191. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo:-

**A. Programu Kuu PN0301: Usimamizi wa Huduma za Maji**

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni:-

Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji na Kuimarisha huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar - ZAWA

**192. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, Wizara imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha udhibiti, usimamizi na matumizi ya Rasilimali za Maji kulingana na Sera ya Maji na mikakati ya kitaifa;
ii. Kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji, miundombinu ya usafirishaji na maabara za maji;
iii. Kushiriki katika makongamano ya Maji Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na kufanya tafiti mbali mbali katika Sekta ya Maji;
iv. Kutoa miongozo na elimu kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira ya vyanzo vya maji;
v. Kutoa miongozo kwa wadau kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na
vi. Kuibua Miradi ya kimkakati katika kuboresha Sekta ya Maji.

**193. Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itatekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo inajukumu la kisheria la kusimamia masuala ya maji hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ZAWA kupitia programu hii imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar – India;
ii. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar (EXIM BANK INDIA);
iii. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upembuzi Yakinifu juu ya Usalama wa Maji na Kina cha Maji chini ya Ardhi (KfW);

iv. Kutekeleza mradi wa Uimarishaji wa huduma za usambazaji wa maji na miundombinu ya maji Mjini (JICA);
v. Kuendeleza kazi za kawaida na matengenezo ya miundombinu ya maji.

194. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 10,870,491,200** kutokana na vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya maji na mapato mengineyo.

195. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezwa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 83,768,109,000** kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 139,811,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 250,022,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 5,863,500,000** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, na **TZS. 77,514,776,000** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo zilizopangwa katika Programu hii.

## B. Programu Kuu PNO302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini

Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati.
ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.

196. **Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya Programu hii, Wizara imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuongeza vyanzo vya uzalishaji umeme kwa kutumia nishati mbadala;
ii. Kuboresha mtandao wa usambazaji na usafirishaji wa umeme Zanzibar;
iii. Kuandaa miongozo ya matumizi ya umeme kwa ufanisi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi na Taasisi za Serikali juu ya miongozo hio;
iv. Kuhamasisha matumizi ya Nishati mbadala na Nishati ya kisasa kwa kupikia;
v. Kuandaa ramani ya kijiolojia;
vi. Kuanzisha maabara ya kijiolojia na madini.

197. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

**a) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)**

198. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuongeza ufanisi kwa kuwapatia huduma bora wateja wetu;
ii. Kuongeza wateja wapya kwa kusambaza huduma ya umeme katika maeneo mapya;
iii. Kuondoa changamoto katika maeneo ambayo yanapata

umeme mdogo pamoja na miundombinu chakavu;

iv. Kuimarisha mifumo ili kupunguza upotevu wa umeme na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato;
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

199. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Umeme (ZECO) linatarajia kukusanya jumla ya **TZS 179.40** Bilioni kupitia vyanzo vyake vya mapato ambayo ni Mauzo ya umeme, Mapato ya huduma nyenginezo, Mchango wa Serikali na Makusanyo ya madeni ya nyuma ya wateja. Aidha, Shirika limekadiria kutumia jumla ya **TZS 178.75** Bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo. Hali kadhalika, Ifikapo tarehe 30 Juni, 2024 Shirika linatarajia kupata bakaa ya jumla ya **TZS 652.99** Milioni.

**b) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)**

200. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ZURA kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za Maji na Nishati;
ii. Kuandaa kanuni na miongozo ya namna ya kudhibiti maji safi na maji machafu pamoja na miongozo ya uunganishaji wa umeme kwenye gridi ya taifa;
iii. Kuimarisha upatikanaji bora, endelevu na salama wa Huduma za Maji na Nishati;
iv. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi;

v. Kuboresha uwezo wa Taasisi wa kudhibiti Huduma za Maji na Nishati;

vi. Kutoa elimu pamoja na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

**201. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imejipangia kukusanya na kutumia jumla ya TZS. 20,061,335,397 kwa kazi za kawaida, Maendeleo na Mchango wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **TZS. 6,461,335,397** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS. 5,600,000,000** kwa ajili ya Kazi za Maendeleo, **TZS. 6,000,000,000** kwa ajili ya Mchango wa Serikali na **TZS. 2,000,000,000** kwa ajili ya mfuko wa kupunguza makali ya bei (stabilization fund).

### c) Idara ya Nishati na Madini

**202. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara kupitia Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali zisizorejesheka imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS. 15,285,400,000.** Makusanyo hayo yanatokana na maombi ya vibali, ada, leseni na faini zitokanazo na malipo ya rasilimali hizo.

**203. Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 41,028,270,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 160,000,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, TZS. 722,297,000 kwa ajili ya mishahara, **TZS. 7,000,000,000** kwa ajili ya malipo ya “retention” na **TZS. 33,145,973,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

## C. Programamu Kuu PNO303: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM

Program hii itakuwa na Programu Ndogo Tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM,
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa WMNM na
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM – Pemba.

**204. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, Wizara imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli zote za Ofisi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao;
ii. Kuandaa na kuratibu mikutano ya Kamati Tendaji, Kamati ya Uongozi, vikao vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani na vikao vya Bodi ya Zabuni;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi;
iv. Kuandaa, Kusimamia na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria na Mipango ya kisekta kwa mujibu wa Vipaumbele vya Wizara;
v. Kuratibu na Kukuza mashirikiano ya Kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara;
vi. Kuratibu na Kufanya tafiti mbali mbali zenye mnasaba na Sekta za Wizara;
vii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Kisekta pamoja na Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (ZanWIP);

viii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za sekta zilizomo ndani ya Wizara kwa upande wa Pemba.

205. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 2,149,570,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo **TZS. 714,289,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **TZS. 1,435,281,000** kwa ajili ya Mishahara.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

206. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza Programu zake na kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Fungu N03 lenye jumla ya **TZS. 126,945,949,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 1,014,100,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS. 8,271,100,000** kwa ajili ya Mishahara, **TZS. 7,000,000,000** kwa ajili ya fedha za "retention" na **TZS. 110,660,749,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Vile vile, naomba idhini ya kukusanya **TZS. 15,285,400,000** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na maliasili zisizorejesheka. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika **Kiambatisho Nambari 11.**

## 7.0 HITIMISHO

207. **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kwa mara nyengine kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna anavyosimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 kwa vitendo na ari yake juu ya kuleta mabadiliko chanya katika Sekta ya Maji na Nishati Zanzibar kupitia miradi mikubwa ya kimkakati aliyoianzisha ndani ya kipindi chake cha Uongozi.
Ni dhahiri tunajivunia mabadiliko makubwa anayoyafanya ndani ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Niwasihi wananchi wenzangu tuendelee kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake za kutuletea maendeleo, tuendelee kuwa wavumilivu tukisubiria neema inayoendelea kutekelezwa kupitia Miradi ya Maendeleo nchini.

208. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika nampongeza Mheshimwa Rais wetu kwa kuweza kutunukiwa Tuzo maalum iitwayo “Global VIP Water Changemakers Awards” kutokana na jitihada zake za kuifanya Zanzibar kuwa nchi ya kwanza Barani Afrika kuanzisha, kuzindua na kuendelea kutoa miongozo juu ya utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (ZanWIP).

209. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za pekee nazileta kwake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Mheshimiwa Yahya Rashid Mamba, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kwahani kwa kuendelea kuishauri Wizara yetu na kufikia mafanikio chanya ya maendeleo ya Taifa letu.

210. **Mheshimiwa Spika,** aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Shaban Ali Othman, Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa namna anavyochapa kazi na kunisaidia katika majukumu ya kuiongoza Wizara hii inayogusa maisha ya kila mwananchi wa Zanzibar.

211. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza kwa dhati wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya Hotuba hii akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Ndugu Joseph John Kilangi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwanajuma Majid Abdullah, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara za Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara.

212. **Mheshimiwa Spika,** kwa hakika ushirikiano wao mzuri na uchapaji kazi mkubwa umesaidia kuweza kuiongoza Wizara hii na kutekeleza majukumu yangu kwa uweledi katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanafaidika na huduma za maji safi na salama, Nishati nafuu na ya uhakika pamoja na upatikanaji wa maliasili zisizorejesheka kwa shughuli mbali mbali za kijamii na kiuchumi.

213. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kushukuru na kuthamini michango na ushirikiano kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi wakiwemo Taasisi ya Ufuatiliaji wa Utendaji Serikali (PDB), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), CRDB Benki, Benki ya Exim ya INDIA, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (EU), IMF, pamoja na Taasisi na Mashirika ya JICA (Japan), GWPSA, GiZ (Ujerumani), NORAD (Norway),

SIDA (Sweden), UNDP, UNICEF, na Wadau wengine wa maendeleo.

214. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii. Aidha, napenda pia kuzishukuru Taasisi za Fedha, Vyombo vya Ulinzi na Usalama bila kusahau vyombo vyote vya habari kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kuendeleza Sekta ya Maji, Nishati na Madini.

215. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kukishukuru Chama changu cha CCM kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (MNEC). Hii ni heshima kubwa kwangu na ninaahidi kuendelea kusimamia kwa vitendo utekelezaji wa Ilani ya CCM.

216. **Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za dhati nizitoe tena kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chake Chake ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kuimarisha maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Pia, nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na Kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa.

Niendelee kuwaahidi na kuwahakikishia kuwa nitazidi kuwatumikia kwa kasi zaidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

217. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba sasa nichukue fursa hii adhimu kuishukuru kwa dhati familia yangu pamoja na watoto wangu kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu yangu.

218. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, kutushauri na hatimae waipitishe Bajeti hii.

219. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**(Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara)**
**Waziri wa Maji, Nishati na Madini**
**Zanzibar.**

# VIAMBATISHO

# Kiambatisho Nam.  1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2022/2023

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2022/2023 (000) SMZ | BAJETI 2022/2023 (000) WAHISANI | BAJETI 2022/2023 (000) JUMLA | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2023 (000) SMZ | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2023 (000) WAHISANI | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2023 (000) JUMLA | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usimamizi wa Huduma za Maji | Kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama | Idara ya Maendeleo ya Maji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 252,000,000 | | 252,000,000 | 152,798,401 | | 152,798,401 | 61 |
| | | | Fedha za Mshahara | 156,716,000 | | 156,716,000 | 136,292,620 | | 136,292,620 | 87 |
| | | **Jumla** | | **408,716,000** | | **408,716,000** | **289,091,021** | **-** | **289,091,021** | **71** |
| | | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | Ruzuku ya Mshahara | 3,608,300,000 | | 3,608,300,000 | 4,397,115,376 | | 4,397,115,376 | 122 |
| | | **Jumla** | | **3,608,300,000** | | **3,608,300,000** | 4,397,115,376 | - | 4,397,115,376 | **122** |
| | Kuimarisha Huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | Fedha za Mradi wa Maendeleo | 22,745,664,000 | 79,940,577,000 | 102,686,241,000 | 2,500,000,000 | 28,558,868,671 | 31,058,868,671 | 30 |
| | | **JUMLA YA PROGRAMU KUU 1** | | **26,762,680,000** | **79,940,577,000** | **106,703,257,000** | **7,186,206,397** | **28,558,868,671** | **35,745,075,068** | **33** |
| Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini | Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Nishati | Idara Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 237,235,000 | | 237,235,000 | 38,611,414 | | 38,611,414 | 16 |
| | | | Fedha za Mshahara | 452,741,000 | | 452,741,000 | 583,549,570 | | 583,549,570 | 129 |
| | | | | **689,976,000** | **-** | **689,976,000** | **622,160,984** | **-** | **622,160,984** | **90** |
| | Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Madini | | Fedha za Matumizi Mengineyo | 48,565,000 | - | 48,565,000 | 12,000,000 | | 12,000,000 | 25 |
| | | **Jumla** | | **48,565,000** | **-** | **48,565,000** | 12,000,000 | | 12,000,000 | **25** |
| | | **Jumla** | | **738,541,000** | **-** | **738,541,000** | **634,160,984** | **-** | **634,160,984** | **86** |
| | Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | Fedha za Mradi wa Maendeleo | 14,729,000,000 | 11,289,780,000 | 26,018,780,000 | | 1,043,242,689 | **1,043,242,689** | **4** |
| | | **Jumla** | | **14,729,000,000** | **11,289,780,000** | **26,018,780,000** | **-** | **1,043,242,689** | **1,043,242,689** | **4** |
| | | **JUMLA YA PROGRAMU KUU 2** | | **15,467,541,000** | **11,289,780,000** | **26,757,321,000** | **634,160,984** | **1,043,242,689** | **1,677,403,673** | **6** |

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2022/2023 (000) | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2023 (000) | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM | Utawala na Uwendeshaji wa WMNM | Utumishi na Uendeshaji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 420,800,000 | | 420,800,000 | 228,582,084 | | 228,582,084 | 54 |
| | | | Fedha za Mshahara | 461,066,000 | | 461,066,000 | 634,008,485 | | 634,008,485 | 138 |
| | | **Jumla** | | **881,866,000** | | **881,866,000** | **862,590,569** | **-** | **862,590,569** | **98** |
| | Uratibu za Mipango , Sera na Utafiti za WMNM | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | Fedha za Matumizi Mengineyo | 253,500,000 | | 253,500,000 | 141,430,401 | | 141,430,401 | 56 |
| | | | Fedha za Mshahara | 91,581,000 | | 91,581,000 | 123,844,240 | | 123,844,240 | 135 |
| | | **Jumla** | | **345,081,000** | | **345,081,000** | **265,274,641** | **-** | **265,274,641** | **77** |
| | Uratibu wa Utekelezaji wa Shughuli za WMNM-Pemba | Afisi Kuu Pemba | Fedha za Matumizi Mengineyo | 300,000,000 | | 300,000,000 | 111,166,000 | | 111,166,000 | 37 |
| | | | Fedha za Mshahara | 346,996,000 | | 346,996,000 | 331,344,430 | | 331,344,430 | 95 |
| | | **Jumla** | | **646,996,000** | | **646,996,000** | **442,510,430** | **-** | **442,510,430** | **68** |
| | | **JUMLA YA PROGRAMU KUU 3** | | **1,873,943,000** | | **1,873,943,000** | **1,570,375,640** | **-** | **1,570,375,640** | **84** |
| | | **JUMLA YA FUNGU N03** | | **44,104,164,000** | **91,230,357,000** | **135,334,521,000** | **9,390,743,021** | **29,602,111,359** | **38,992,854,381** | **29** |

## Kiambatisho Nam. 2: Maeneo yaliyorejeshewa Huduma ya Maji Safi na Salama

| | UNGUJA | | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1. | Donge-nje, | 24.Mkwajuni-Kongwe | 1. Wete (13) |
| 2. | Donge ndani | 25.Jendele-Marumbi | 2. Mkoani (22) |
| 3. | Kizimkazi | 26.Kaburi-Kikombe | 3.Chake chake (26), |
| 4. | Chaani-Tasaf | 27.Mwera-Mchomeke -K401 | 4. Micheweni (9) |
| 5. | kwa Bint Amrani | 28.Bambi- pongwe | |
| 6. | Tazari- Mazingira, | 29.Mchomeke -No 1 | |
| 7. | Chumbuni, | 30. Kidutani | |
| 8. | Mkwajuni, | 31.Bumbwi sudi -Ghana | |
| 9. | Kaburi- Kikombe RAK | 32. Paje | |
| 10. | Jendele- Marumbi, | 33.Mbweni-ZSSF | |
| 11. | Mkwajuni kwa Mzungu, | | |
| 12. | Ndijani – Mjonga, | | |
| 13. | Jambiani –Kivuli, | | |
| 14. | Kaburi Kikombe U 27 | | |
| 15. | Kianga- Nje | | |
| 16. | Mchomeke | | |
| 17. | Paje | | |
| 18. | Msikiti Mzuri | | |
| 19. | Mjonga | | |
| 20. | Jambiani-Kivuli | | |
| 21. | Dimani BH | | |
| 22. | Donge mchina 1 | | |
| 23. | Bumbwisudi NB 8 | | |

## Kiambatisho Nam. 3: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya usafishaji wa visima

| Nam. | UNGIJA | PEMBA |
|---|---|---|
| 1. | Kianshanga – Mzungu | 1.) Kijuki |
| 2. | Welezo | 2.) 2.) Junguni |
| 3. | Dunga Rak kwa Abdallah rashid | 3.) Konde- Skuli |
| 4. | Kaburi kikombe u- 27 | 4.) Ukutini |
| 5. | Fuoni – Birikani | 5.) Mahuduthi |
| 6. | Kizimbani –RAK | 6.) Sinongone |
| 7. | Msikiti –Mzuri | 7.) Kiwani- 1 |
| 8. | Bumwisudi | 8.) Kiwani- 2 |
| 9. | Mangapwani | 9.) Kengeja- Mjiweni |
| 10. | Mbuzini | 10.) Kengeja kaani |
| 11. | Mwera- Pongwe | 11.) Mtambile –Skuli |
| 12. | Kitope- Skuli | 12.) Mtambile –Muwanda |
| 13. | Kibonde –mzungu | 13.) Mgagadu |
| 14. | Mbweni ZSSF | 14.) Mgagadu kwa Mkoba |
| 15. | Chunga –jangamizini | 15.) Pagali |
| 16. | Maungani uwanja wa mpira | 16.) Amani- Rodi |
| 17. | Kisakasaka | 17.) Ziwani |
| 18. | Dimani njia kuu | 18.) Ngwambwa -1 |
| 19. | Bummbini - Misufini | 19.) Ngambwa – 2 |
| 20. | Mjonga | 20.) Bi Mtumwa -2 |
| 21. | Muembe- Makumbi | 21.) Chanjaani – 2 |
| 22. | Tazari Jendele- Marumbi | 22.) Matuleni – 1 |
| 23. | Mkundunchi -Nurssary | 23.) Chanjaani- 1 |
| 24. | Welezo no 1 | 24.) Matuleni – 2 |
| 25. | Welezo U 64 | 25.) Sharifu Ali -2 |
| 26. | Muembe- Mkumbi | 26.) Mjananza |
| 27. | Migombani- masauni | 27.) Bi Mtumwa-1 |
| 28. | Kianga kwa Mzee Jma | |
| 29. | Selemu | |
| 30. | Mwachealale | |
| 31. | Dimani | |
| 32. | Shakani kwa Mussa elimu | |
| 33. | Ndijani- Mjonga | |

**Kiambatisho Nam. 4: Dhana za Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Nishati iliyotayarishwa kwa ajili ya kuombewa ufadhili**

i. *Mradi wa Upembuzi yakinifu wa umeme wa upepo (Feasibility study of wind);*
ii. *Mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji wa umeme Pemba (Rehabilitation of power distribution infrustructures);*
iii. *Utafiti wa upotevu wa umeme (Power loss study);*
iv. *Mradi wa majiko sanifu (Improved cooking stoves);*
v. *Mradi wa kuongeza umeme Unguja kutoka Tanzania Bara kwa kutumia waya wa bahari wa kiwango cha megawati 200 (200 MW Submarine Cable);*
vi. *Mradi wa kuongeza umeme Unguja kutoka Tanzania Bara kwa kutumia Bomba la Gesi;*
vii. *Mradi wa kuongeza umeme Pemba kutoka Tanzania Bara kwa kutumia waya wa bahari wa kiwango cha megawati 100 (100 MW Submarine Cable).*

## Kiambatisho Nam. 5: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023

| Nam. | Eneo | Nam | Eneo |
|---|---|---|---|
| 1 | Fuoni kipungani | 1 | Konde chanjaani |
| 2 | Koani | 2 | Vitongoji Vijijini |
| 3 | Chuini Ziwani | 3 | Mabweni Mtambile |
| 4 | Umbuji Kusini (Uwandani) | 4 | Pujini Kijili |
| 5 | Umbuji Kaskazini | 5 | Penjewani |
| 6 | Mgeni Haji | 6 | Kimbu Pujini |
| 7 | Makunduchi tangini | 7 | Pujini Kibaridi |
| 8 | Welezo msikiti ngamia | 8 | Mkamandume |
| 9 | Matemwe Kizimiani | 9 | Mchangani |
| 10 | Kizimkazi Dimbani | 10 | Mtambile skuli |
| 11 | Tunguu Istiqama | 11 | Vitongoji Marekani |
| 12 | Mitakawani | 12 | Tangaani |
| 13 | Maungani Uwandani | | |
| 14 | Fuoni mambo sasa | | |
| 15 | Jumbi | | |
| 16 | Kianga | | |
| 17 | Kwarara kandahari | | |
| 18 | Bambi ya Bondeni | | |
| 19 | Michamvi | | |
| 20 | Fuoni viwanja vya walimu | | |
| 21 | Upenja JKU | | |
| 22 | Charawe | | |
| 23 | Bungi Usalama | | |
| 24 | Mahad Istiqama | | |
| 25 | Darajani | | |
| 26 | Nungwi baobao | | |
| 27 | Paje Garage | | |
| 28 | Mwera batini | | |
| 29 | Paje hospitali | | |
| 30 | Makunduchi kajengwa | | |
| 31 | Fuoni 2005 | | |
| 32 | Nungwi njia ya maafa | | |
| 33 | Tunguu mtundani | | |
| 34 | Kibele njia ya kwa Dr Shein | | |
| 35 | Kazole kwa Gube | | |
| 36 | Kwanyanya | | |
| 37 | Dole Angola | | |

# Kiambatisho Nam. 6: Vijiji viliyopelekewa huduma ya umeme Unguja na Pemba

| Nam. | UNGUJA | Nam. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1 | Bungi Kichungwani | 1 | Bandani Kiuyu |
| 2 | Mtende Cheju | 2 | Blue Wawi Chimbe |
| 3 | Koani Sanda Mkobani | 3 | Mnarani makangale |
| 4 | Mwanyanya Chato | 4 | Utasini makombeni |
| 5 | Miwani Kinoni | 5 | Ngagu mkumbuu |
| 6 | Mchangani Michongomani | 6 | Kitwea |
| 7 | Bumbwini Kiwarani | 7 | Kizungu Mkoani |
| 8 | Dole Ndunduke juu ya Kilima | 8 | Mkinduni |
| 9 | Chuini Ziwani | 9 | Kipange |
| 10 | Pale Kiongele | 10 | Uwaani Tumbe |
| 11 | Michamvi karafuu | 11 | Wingwi Mlindo |
| 12 | Mchangamle Fukuchani | 12 | Muundoni Shumba |
| 13 | Pangeni | 13 | Kiimbini |
| 14 | Kianga Ijitimai | 14 | Mtadoda |
| 15 | Bwereu Kisima cha maji | 15 | Mgelele |
| 16 | Binguni kwa bodi | 16 | Kangani |
| 17 | Kiboje Uchukuni | 17 | Mkanyageni |
| 18 | Mtule | 18 | Mapape |
| 19 | Muyuni Karbara | 19 | Ngezi |
| 20 | Kijiji cha Kisakasaka | 20 | Kitokame |
| 21 | Donge kiongwe kidogo | | |
| 22 | Panga tupu Hospital | | |
| 23 | Mbuzini Hospital | | |
| 24 | Fukuchani Mchangamle | | |
| 25 | Jimbo la Chaani | | |
| 26 | Muyuni 'C' KVZ | | |
| 27 | Pete Mashambani | | |
| 28 | Donge Kipange | | |
| 29 | Pangeni Kiamboni | | |
| 30 | Mkwajuni Kichangani | | |
| 31 | Pale kiongele wananchi | | |
| 32 | Unguja Ukuu Kaebona | | |
| 33 | Binguni | | |
| 34 | Mwakaje Mashimo ya mchanga | | |
| 35 | Muungoni Mkuku mashambani | | |
| 36 | Kiboje uwandani | | |
| 37 | Ghana kirundunda | | |
| 38 | Kizimbani tomokani | | |
| 39 | Pete kiungani | | |

## Kiambatisho Nam. 7: Hali ya Uingizwaji na Matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa

| HALI YA UINGIZWAJI NA MATUMIZI YA MAFUTA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA KUANZIA JULAI HADI MACHI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 ( LITA) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWEZI** | **YALIYOINGIZWA/MATUMIZI** | **PETROLI** | **DIZELI** | **MAFUTA YA TAA** | **JET A-1** | **JUMLA** |
| JULAI 2022 | Yaliyoingizwa | 8,176,142 | 3,852,905 | 204,958 | 3,790,701 | **16,024,706** |
| | Matumizi kwa mwezi | 5,969,250 | 4,125,810 | 251,500 | 4,354,200 | **14,700,760** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **192,556** | **133,091** | **8,113** | **140,458** | **474,218** |
| AGOSTI 2022 | Yaliyoingizwa | 8,275,022 | 6,622,969 | 252,052 | 3,799,424 | **18,949,467** |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,131,300 | 5,842,724 | 306,104 | 3,828,000 | **19,108,128** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **294,558** | **188,475** | **9,874** | **123,484** | **616,391** |
| SEPTEMBA 2022 | Yaliyoingizwa | 8,234,598 | 5,675,174 | | 1,895,362 | **15,805,134** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,514,107 | 5,547,116 | 244,100 | 1,804,000 | **16,109,323** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **283,804** | **184,904** | **8,137** | **60,133** | **536,977** |
| OKTOBA 2022 | Yaliyoingizwa | 6,123,213 | 4,056,239 | 496,052 | 3,707,161 | **14,382,665** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,624,445 | 5,658,119 | 238,643 | 3,124,000 | **17,645,207** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **278,208** | **182,520** | **7,698** | **100,774** | **569,200** |
| NOVEMBA 2022 | Yaliyoingizwa | 12,523,573 | 6,966,640 | 412,476 | 3,796,926 | **23,699,615** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,423,447 | 5,584,514 | 225,995 | 4,004,000 | **18,237,956** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **280,782** | **186,150** | **7,533** | **133,467** | **607,932** |
| DISEMBA 2022 | Yaliyoingizwa | 5,706,185 | 5,260,418 | | 3,803,105 | **14,769,708** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,791,461 | 5,626,348 | 140,948 | 3,250,000 | **17,808,757** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **283,596** | **181,495** | **4,547** | **104,839** | **574,476** |
| JANUARI 2023 | Yaliyoingizwa | 10,515,826 | 5,352,361 | 1,102,159 | 6,013,967 | **22,984,313** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,902,830 | 5,670,219 | 225,218 | 5,444,000 | **20,242,267** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **287,188** | **182,910** | **7,265** | **175,613** | **652,976** |
| FEBRUARI 2023 | Yaliyoingizwa | 9,153,940 | 6,593,635 | 485,888 | 3,813,773 | **20,047,236** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,306,361 | 5,276,027 | 154,528 | 4,180,000 | **17,916,916** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **296,656** | **188,430** | **5,519** | **149,286** | **639,890** |
| MACHI 2023 | Yaliyoingizwa | 9,576,033 | 5,905,800 | 0 | 3,810,346 | **19,292,179** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,960,483 | 6,507,460 | 205,327 | 3,520,000 | **19,193,270** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | **289,048** | **209,918** | **6,623** | **113,548** | **619,138** |

***Chanzo: ZURA 2023***

**Kiambatisho Nam. 8: Mwenendo wa bei halisi na bei elekezi katika soko la Zanzibar (TZS) kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023**

| BEI ZILIZOTANGAZWA KUANZIA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MWEZI | TAREHE YAKUTANGAZWA | BEI ILIYOTANGAZWA | | | |
| | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA NDEGE | MAFUTA YA TAA |
| JULAI 2022 | 08.07.2022 | 2,980 | 2,990 | 2,743 | 2,921 |
| AGOSTI 2022 | 08.08.2022 | 2,980 | 2,990 | 3,147 | 2,921 |
| SEPTEMBA 2022 | 09.09.2022 | 2,980 | 2,990 | 2,681 | 2,921 |
| OKTOBA 2022 | 08.10.2022 | 2,980 | 2,990 | 2,743 | 2,921 |
| NOVEMBA 2022 | 08.11.2022 | 2,980 | 2,990 | 3,147 | 2,921 |
| DISEMBA 2022 | 08.12.2022 | 2,980 | 2,990 | 2,681 | 2,921 |
| JANUARI 2023 | 08.01.2023 | 2,980 | 2,990 | 2,681 | 2,921 |
| FEBRUARI 2023 | 08.02.2023 | 2,880 | 2,990 | 2,681 | 2,921 |
| MACHI 2023 | 08.03.2023 | 2,880 | 2,980 | 2,681 | 2,921 |

***Chanzo: ZURA 2023***

## Kiambatisho Nam. 9: Idadi ya Vituo vya Mafuta vilivyopo Nchini

| | WILAYA | GAPCO | UGL | ZPL | PUMA | SERIKALI | BINAFSI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| UNGUJA | MJINI | 5 | 2 | 2 | | | 3 | **12** |
| | MAGHARIBI "A" | 3 | 3 | 2 | | | 4 | **12** |
| | MAGHARIBI "B" | 1 | 2 | 3 | 1 | | 9 | **16** |
| | KATI | 1 | 3 | 2 | | | 4 | **10** |
| | KUSINI | 0 | 3 | 1 | | | 7 | **11** |
| | KASKAZINI "A" | 2 | 1 | 3 | | | 6 | **12** |
| | KASKAZINI "B" | 1 | 1 | 0 | | | 2 | **4** |
| | **JUMLA NDOGO** | **13** | **15** | **13** | **1** | **0** | **35** | **77** |
| PEMBA | MICHEWENI | | | | | | 4 | **4** |
| | WETE | | | | | 1 | 3 | **4** |
| | CHAKECHAKE | | | 1 | | 2 | 4 | **7** |
| | MKOANI | | | | | | 4 | **4** |
| | **JUMLA NDOGO** | | **0** | **1** | **0** | **3** | **15** | **19** |
| **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | | **13** | **15** | **14** | **1** | **3** | **50** | **96** |

***Chanzo: ZURA 2023***

## Kiambatisho Nam. 10: Kiwango cha Gesi iliyoingizwa na iliyotumika Nchini (Kg)

| MWEZI/KAMPUNI | ORXY GAS TANZANIA LIMITED | | LAKE GAS TANZANIA LIMITED | | TAIFA GAS TANZANIA LIMITED | | TP COMPANY LIMITED - V- GAS | | ALNABAHAN GAS SUPPLY -O-GAS | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2022/23** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** |
| JULAI 2022 | 458,640 | 440,555 | 56,800 | 39,711 | 55,500 | 87,876 | | | 25,000 | 2,500 |
| AGOSTI 2022 | 520,080 | 551,302 | 54,040 | 52,119 | 35,250 | 83,763 | | | 21,000 | 21,000 |
| SEPEMBA 2022 | 498,900 | 488,661 | 36,380 | 46,154 | 57,370 | 82,617 | | | 24,500 | 24,500 |
| OKTOBA 2022 | 466,045 | 491,355 | 53,020 | 45,182 | 82,365 | 80,603 | 105,480 | 93,276 | 27,000 | 27,000 |
| NOVEMBA 2022 | 472,955 | 461,955 | 35,740 | 36,519 | 51,320 | 57,268 | 73,740 | 89,930 | 28,500 | 28,500 |
| DISEMBA 2022 | 459,060 | 494,656 | 35,800 | 39,030 | 99,278 | 86,100 | 78,670 | 79120 | 26,500 | 26,500 |
| JANUARI 2023 | 451,320 | 460,924 | 34,980 | 31,694 | 75,654 | 78,328 | 59,200 | 65,300 | 3,000 | 3,000 |
| FEBUARI 2023 | 471,600 | 435,586 | 57,660 | 35,109 | 39,255 | 56,877 | 72,540 | 69,600 | 4,500 | 4,500 |
| MACHI 2023 | 537,000 | 564,573 | 35,600 | 33,001 | 122,435 | 97,940 | 72700 | 71100 | 5,500 | 5,500 |
| **JUMLA NDOGO** | **4,335,600** | **4,389,567** | **400,020** | **358,519** | **618,427** | **711,372** | **462,330** | **468,326** | **165,500** | **143,000** |

***Chanzo: ZURA 2023***

# Kiambatisho Nam. 11: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

| | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA** | **RUZUKU YA MSHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **MHISANI** | **RUZUKU** | **JUMLA** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | **250,022,000** | **5,863,500,000** | **139,811,000** | **24,504,964,000** | **52,934,812,000** | **75,000,000** | **83,768,109,000** |
| Usimamizi na Uratibu wa wa Huduma za Maji | 250,022,000 | 5,863,500,000 | 139,811,000 | 24,504,964,000 | 52,934,812,000 | 75,000,000 | 83,768,109,000 |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **722,297,000** | **-** | **7,160,000,000** | **24,200,000,000** | **8,878,345,000** | **67,628,000** | **41,028,270,000** |
| **MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA** | 722,297,000 | - | 117,025,400 | 24,200,000,000 | 8,878,345,000 | 67,628,000 | 33,985,295,400 |
| Usimamizi na Uratibu wa wa Huduma za Madini | | | 42,974,600 | | | | 42,974,600 |
| Uendeshaji wa Huduma za Madini (Retention) | | | 7,000,000,000 | | | | 7,000,000,000 |
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WMNM** | **1,435,281,000** | **-** | **714,289,000** | **-** | **-** | **-** | **2,149,570,000** |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 655,812,000 | - | 353,100,000 | - | - | - | 1,008,912,000 |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM | 146,107,000 | - | 160,189,000 | - | - | - | 306,296,000 |
| Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM-Pemba | 633,362,000 | - | 201,000,000 | - | - | - | 834,362,000 |
| **JUMLA KUU** | **2,407,600,000** | **5,863,500,000** | **8,014,100,000** | **48,704,964,000** | **61,813,157,000** | **142,628,000** | **126,945,949,000** |